# Nipashe

Jumamosi Julai 6, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579963

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

w.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Waziri Lugola atoa neno zito makanisa na misikiti

UKURASA 3




UKURASA 13

# Gharama matibabu Ndugai zazua jambo

• **Wazee** Chadema wataka ripoti itue bungeni, washangazwa na matumizi Dola milioni 12, wasema... *Endelea ukurasa 2*



Rais Dk. John Magufuli akizungumza jambo na mgeni wake Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wakipita kwenye Gadi ya Heshima iliyoandaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita jana, kwa ziara binafsi ya siku mbili. **PICHA: IKULU**

## Adaiwa kujiua kisa madeni

UKURASA 2

# JPM, Kenyatta watema nyongo

• **Wasema** Tanzania, Kenya ni ndugu, hakuna wa kuwatenganisha... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **MKWABI AFUNGUKA SINTOFAHAMU SIMBA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Gharama matibabu Ndugai zazua jambo

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Wazee wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wamemwibukia spika wa Bunge, Job Ndugai, huku wakitaka ripoti ya gharama za matibabu ya kiongozi huyo wa chombo cha kutunga sheria alipokuwa India, iwasilishwe bungeni.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hashim Issa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akidai kuwa ndani ya matibabu hayo kuna harufu ya ufisadi.

Issa alidai kuwa matibabu ya Spika Ndugai yalitumia dola za kimarekani milioni 12 na kwamba huo ni ufisadi uliolenga kuvusha fedha ambazo ni kodi za Watanzania.

"Tunataka kuona ripoti zote zinawasilishwa bungeni, vikiwamo vyeti vya matibabu na madaktari walifanya operesheni," alisema.

Alidai kuwa Spika Ndugai alikwenda nchini India kutibiwa ingawa hawajui alikuwa anasumbuliwa na nini.

"Matokeo yake alivyorudi Tanzania akasema ametumia Dola za kimarekani milioni 12. Maradhi gani hayo? Kafanya opereshenі ngapi? Alikwenda hospitali ya aina gani mpaka alipe dola milioni 12. Hakuna duniani, huo ni ufisadi.

"Hiyo ilikuwa njia ya kuvusha fedha ambazo ni kodi za Watanzania kutumia kisingizio cha maradhi kwenda hospitali, kumbe kavusha fedha," alidai huku akisisitiza Baraza la Wazee Chadema, linataka kuona ripoti zote zinawasilishwa bungeni.

"Ripoti ya Spika Ndugai, tunataka vyeti vyote vya hospitali, hesabu ya madaktari, alifanyiwa operesheni ngapi. Tunataka hesabu kamili ya miezi yote ya matibabu kama zimefika Dola za kimarekani milioni 12," alisema.

Aprili 14, mwaka huu, Spika Ndugai akijibu swali la gharama ya matibabu yake nje ya nchi wakati akizungumza na waandishi wa habari, alisema kuugua kwake kumelisababishia taifa fedha nyingi, hawezi kujua.

"Labda ningekufa watu wangefurahi. Katika matibabu yoyote yale, tunawatibu watu hatuangalii thamani ya mtu na kiwango cha fedha kilichotumika. Kinachoangaliwa kama kuna matumizi mabaya ndani ya matumizi hayo," alisema.

"Nilitibiwa mwaka 2015/16 na hesabu hizo ni za 2017/18. Unajua tena mtu akibanwa anatafuta sababu huku na kule. Wanaotibiwa ni wengi na hospitali niliyokwenda kutibiwa ni ya kawaida. Nilikutana na Watanzania wa kila aina, wa aina zote, tunapishana huyu anakwenda kwa daktari huyu, mwingine huyu, sijawahi kwenda hospitali ya New York (Marekani), Ujerumani, naenda India ambako ndiko Watanzania wanakotibiwa," aliongeza.

Aprili, mwaka jana, Spika Ndugai alirejea nchini akitokea India alikokuwa akipatiwa matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimsumbua kwa miezi kadhaa.



Umati wa wananchi wakiwa katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Magufuli, Kenyatta watema nyongo

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli na mwenzake wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wamesema watu wa nchi hizo ni ndugu na kamwe hawezi kutokea mtu wa kuwagawa.

Marais hao waliyasema hayo jana wilayani Chato mkoani Geita baada ya Rais Kenyatta kuwasili Tanzania kwa ziara binafsi ya siku mbili.

Akizungumza na Watanzania, Rais Kenyatta alisema: "Unajua wanasiasa shida yao wengine wanaongea bila kufikiria. Mtu anajiona mahali ameishi hajatoka kijijini kwake anafikiri ndiyo mwisho wa dunia.

"Wengine wanaropoka mambo hayapo. Unawezaje kumwambia Mtanzania huwezi kufanya biashara Kenya? Wawezaje kumwambia Mtanzania huwezi kutembea Kenya? Wawezaje kumwambia Mtanzania huwezi kwenda kutafuta bibi (mke) Kenya, inawekezana kweli?" alihoji.

Pia Kenyatta alisema mtu hawezi kumzuia Mkenya kwenda Tanzania kufanya biashara yake, kwenda kumtembelea jirani au rafiki yake au akiwa amemwona mtoto Chatu.

"Hii ndiyo Afrika Mashariki ambayo tunaitaka, siyo ya watu wenye fikra ndogo za zamani za kikabila na za ujinga," alisema.

Rais Kenyatta alisema yupo Tanzania kwa sababu ya uhusiano mwema uliopo kati ya nchi hizo mbili.

"Tupo hapa kwa sababu ya uhusiano mwema. Kama nchi jirani, Mungu alituambia ya kwamba waweza kuchagua rafiki, lakini si jirani, jirani ni yule Mungu amekupatia, hakuna kitu kizuri kama furaha, una jirani uliyechaguliwa na Mungu lakini huyo jirani ni rafiki," alisema.

Kenyatta alisema wapo hapo ili kuimarisha urafiki huo, kusisitiza kuwa mataifa hayo mawili yamebarikiwa na Mungu kwa rutuba na mali nyingi.

"Tuna wananchi wema, wanajuana, tunazungumza lugha moja, uende Namanga hawa ni majirani kwa lugha ya jirani na kitaifa, ufike upande wa Pwani ni ndugu na jamii moja," alisema.

"Je, wanaweza kututenganisha sisi kweli? Hawawezi. Ndipo sisi kama watoto wa Afrika Mashariki tunasema tunastahili tuwe kama sisi, viongozi tunafanya yote tunayoweza kuhakikisha tunaondoa vikwazo vyote ambavyo vinazuia watu wetu kutembeleana, kufanya

INAENDELEA UK. 8

## Adaiwa kujiua kisa madeni

**Na Beatrice Moses**

MWANAMUME aliyetambulika kwa jina la Evarist Massawe, anadaiwa kujiua na kuacha ujumbe akielezea sababu za kuchukua uamuzi huo kuwa ni kutapeliwa Sh. milioni sita na kujikuta akielemewa na madeni.

Massawe, alikuwa mgane, alikuwa mfanyabiashara na mkazi wa mtaa wa Ukombozi, Kata ya Saranga, Ubungo jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya mashuhuda walisema Massawe alijiua siku kadhaa zilizopita bila kugundulika hadi harufu kali ilipojitokeza juzi na kushtua majirani zake.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ukombozi, Yessaya Mande, alisema alipigiwa simu juzi saa moja usiku alipokuwa amejipumzisha nyumbani kwake na baada ya kufika eneo la tukio, alibaini kwamba kuna mtu amekufa.

"Niliambiwa niingie ndani ya nyumba ya Massawe ili nijue kuna tatizo gani. Baada ya kuingia, nilikuta harufu kali na nilipotazama vizuri niliona mwili wake ukiwa umevimba na kuna damu zimesambaa hali ilikuwa inatisha nikatoka haraka kule chumbani," alisema Mande.

Alisema polisi walipewa taarifa na walifika na kuingia kwenye nyumba hiyo kisha baada ya kusogeza mwili ili kuuondoa ndipo walipoona barua ambayo inasadikiwa kuwa iliandikwa na Massawe kabla ya kujiua.

" Katika barua ile aliandika mambo mengi lakini alieleza kuwa uamuzi wake wa kujiua unatokana na kudhulumiwa Sh. milioni sita na wakala wa Vodacom aliyemtaja kwa jina la Raphael, wakati yeye ana madeni mengi ikiwamo kudaiwa na benki na watu binafsi," alisema Mande.

Alisema kuwa Massawe katika barua yake hiyo alidai kwamba kuna mtu anayemdai Sh. 200,000 ambaye amekuwa akimsumbua ambaye hakuwa akiamini kuwa kuna mahali alikuwa akidai fedha ambazo ametapeliwa.

"Pia pamoja na maelezo mengine, Massawe aliagiza mwili wake usisafirishwe kwenda kuzikwa kwao Rombo mkoani Kilimanjaro, bali azikwe kwenye makaburi ya hapa Saranga," alisema Mande.

Baadhi ya majirani ambao hawakuwa tayari majina yao kutajwa kwenye gazeti, walieleza kwa nyakati tofauti kuwa Massawe alikuwa na wakati mgumu hasa baada ya mkewe kufariki dunia miaka kadhaa iliyopita, hivyo alikuwa na maisha ya upweke.

Kamanda wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, akizungumza na gazeti hili alisema bado hajapata taarifa rasmi kuhusu tukio hilo, hivyo akaahidi kulifuatilia.

HABARI KITAIFA



Mfanyabiashara wa mbuzi akiwakokota kwaajili ya kwenda kuwaonyesha wateja, katika mnada wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. Mbuzi mmoja aliuzwa kwa bei ya 65,000/- hadi 170,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Lugola atoa neno kwa makanisa na misikiti

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ametangaza kuchukulia hatua makanisa na misikiti ambayo haitakwenda kufanyiwa uhakiki.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji cha Mwiseni, Kata ya Butimba, Jimbo la Mwibara, Bunda, mkoani Mara, Lugola alisema uhakiki huo unalengo kuangalia taasisi hizo kama zinakwenda sawa kama Sheria ya Usajili inavyoelekeza.

"Serikali iliona ni lazima ifanye uhakiki kwanza kwa lengo la kujua taasisi hizi zinakwenda sawa na sheria za usajili, ndiyo maana hatukuendelea na usajili wa makanisa na misikiti pamoja na taasisi za kiroho," alisema.

Lugola ambaye ni Mbunge wa Mwibara, alitaka taasisi hizo za kidini ziendeshwe kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa na si kujihusisha na mambo ambayo hayahusiki.

Akizungumzia kuhusu vitambulisho vya taifa, Lugola alisema hakuna mwananchi atakakikosa na tayari alishawasiliana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kuwataka watoe namba kwa wakati ili wananchi wafanyiwe usajili wa simu zao za mkononi.

## NEC yatangaza uchaguzi kumrithi Lissu

**Na Mary Geofrey**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza uchaguzi mdogo katika Jimbo la Singida Mashariki, mkoani Singida utakaofanyika Julai 31, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, alitangaza hatua hiyo jana jijini Dar es Salaam na kusema kuwa ratiba inatokana na barua ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, inayoeleza kuwa aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Tundu Lissu (Chadema), amepoteza sifa ya kuwa mbunge.

Katika taarifa ya Spika Ndugai, alitaja sababu za Lissu kuvuliwa ubunge kuwa ni kushindwa kuwasilisha tamko la mali na madeni na kutohudhuria mikutano saba mfululizo bila ruhusa ya Spika.

"Tumezingatia matakwa ya kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura ya 343, kutoa taarifa kwa umma kuhusu uwapo wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Singida Mashariki," alisema Jaji Kaijage.

Jaji Kaijage alisema fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Julai 13 na 18 mwaka huu, na uteuzi wa wagombea utafanyika Julai 18.

Alisema kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia Julai 19 hadi 30 na siku ya uchaguzi itakuwa Julai 31, mwaka huu.

Aidha, alivikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na tume hiyo wakati wa kipindi chote cha uchaguzi huo mdogo.

Wiki iliyopita, Spika Ndugai katika taarifa yake ya kuahirisha mkutano wa Bunge la Bajeti mjini Dodoma, alitangaza kumvua ubunge Lissu wakati akiwa ameshawasilisha taarifa hiyo kwa NEC kwa ajili ya kuitisha uchaguzi mdogo wa jimbo hilo.

Ndugai alisema kanuni za bunge na katiba ya nchi zinataka mbunge huyo avuliwe ubunge kwa kutotimiza masharti ya kuendeleza ushiriki wake katika shughuli za bunge.

Lissu ambaye alikuwa mnadhimu wa kambi ya upinzani bungeni kuanzia 2015 alikwenda nje ya nchi tangu aliposhambuliwa kwa risasi na watu wasiyojulikana akiwa nyumbani kwake mjini Dodoma Septemba, 2017.

Baada ya kunusurika katika shambulizi hilo Lissu alisafirishwa hadi Nairobi, Kenya kwa matibabu na dharura na baadaye nchini Ubelgiji ambako amekuwa akipata matibabu kwa miezi kadha sasa.

Mwanzoni mwa mwaka huu, Lissu akiwa ameanza kupata nafuu kubwa alitembelea nchi kadhaa ikiwa ni pamoja na Uingereza, Marekani na kuilaumu serikali kwa kushindwa kupata ufumbuzi kuhusu shambulizi dhidi yake.

Mwanasiasa huyo pia alitangaza mwezi uliopita kuwa anapanga kurejea nchini Septemba mwaka huu ikiwa ni miaka miwili tangu kunusurika shambulizi la kutaka kumuua.

## Tibaijuka atangaza kung'atuka ubunge

**Na Mary Geofrey**

MBUNGE wa Muleba Kusini (CCM), Profesa Anna Tibaijuka, ametangaza kujiweka kando katika masuala ya siasa huku akisema hatagombea tena ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Katika mahojiano maalum na 'blog' ya Millard Ayo, Prof. Tibaijuka alisema anastaafu kwa sababu yeye ni kizazi cha Mwalimu Julius Nyerere ambaye aliwafundisha kung'atuka.

"Mimi 2020 ninastaafu, ninang'atuka kwa sababu sisi ni kizazi cha Mwalimu Nyerere na katika vitu alivyotufundisha ni kung'atuka," alieleza Prof. Tibaijuka katika mahojiano yake hayo. Alipouliza kama sababu ni kuhofia kushindwa katika uchaguzi ujao, alisema hakuna anyemhofia kwa sababu mwaka 2015 alipita katika uchaguzi licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa.

"Katika uchaguzi wa 2015, Muleba Kusini pamoja na kampeni ya Escrow bado nilipita kidedea. Kwa kweli nawashukuru wananchi wa Muleba. Ni watu wanaotafuta maendeleo, wana kiu ya maendeleo," alisema Prof. Tibaijuka na kuongeza kuwa:

"Ninaposema nastaafu ubunge haimaanishi kwamba nastaafu Muleba, hivi ni vitu viwili tofauti. Mimi ninastaafu uwakilishi, Bunge letu hili lingekuwa Seneti ningesema nitaendelea," alisema Prof. Tibaijuka

Alisema kwa sababu Bunge linalinda maslahi mapana ya umma hawezi kuwania tena ingawa anaamini atapatikana mwakilishi mzuri kutoka jimbo hilo.

Alisema mwaka 2015 kulikuwa na kampeni chafu dhidi yake lakini wananchi wa Muleba waliamuamini katika kipindi chote cha miaka 10 hivyo anaamua kung'atuka kwa utashi wake.

"Mimi kama kupigwa chini ningepigwa chini mwaka 2015. Asiyekubali kushindwa si mshindani, kwa hiyo mimi sistaafu kwa ajili ya hofu, kwanza Muleba anayenishinda ni nani? Ni Mwenyezi Mungu peke yake. "Kwa kipindi cha miaka 10 nimejifunza, nimeelewa matatizo ya wananchi na wakati ule nilipotoka Umoja wa Mataifa, nilikuja na nia moja ya kujifunza kwamba taifa letu lina tatizo gani na tufanye nini ili tuweze kusogea mbele," alisema.

"Kwa hiyo hata bungeni ninaposimama, nikiona kitu hakijakaa sawa huwa sisimami kiitikadi. Pia sitaki siasa ambao hauna mantiki," alisema Prof. Tibaijuka.

Mwanasiasa huyo na mchumi nguli, aliwaasa wagombea ambao watataka kuwania nafasi hiyo katika jimbo hilo kuwa wastaarabu na kuacha pupa kwa sababu wananchi wake ni waelewa.

"Wanaotaka kugombea waje kwa adabu wasije kwa jazba, fitina na mbinde," alisema Prof. Tibaijuka.

Prof. Tibaijuka pia aliahidi kujikita katika kusaidia wanawake na wasichana ambao hawafahamu haki zao kwa ajili ya kuepuka matukio ya ukatili wa kijinsia na mauaji ya vikongwe. Alisema pia katika umri wake wa kustaafu ubunge akiwa jimboni kwake, atajikita kutoa elimu ya kujitambua kwa wasichana na wanawake ambao hawazifahamu haki zao katika jimbo hilo.

# Kortini akidaiwa kumuua mkewe

**Na Happy Severine,** MASWA

MKAZI wa Mtaa wa Majengo katika mji wa Maswa mkoani Simiyu, Emanuel Nyandu (35), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Maswa kwa tuhuma za mauaji ya Mkewe, Julieth Josephat (30) aliyekuwa mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Shanwa Seminari, wilayani hapa.

Akisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Fredrick Lukuna na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Inspekta Nassib Sweddy, ilidaiwa kuwa Nyandu alifanya mauaji hayo Julai 2, mwaka huu saa 9:00 mchana wakiwa katika nyumba yao waliyokuwa wakiishi kama wanandoa.

Sweddy alidai kuwa mshitakiwa ambaye alikuwa na ugomvi na mkewe, alimchoma kwa kutumia kitu chenye ncha kali kichwani mara tano, shingoni mara mbili, tumboni mara nne na kisha kumpiga kwa nyundo kichwani na kumsababishia kifo.

Alidai kuwa wakati mshtakiwa akifanya mauaji hayo, hakukuwa na mtu mwingine katika nyumba yao licha ya kuishi wakiwa na mtoto wao mdogo na binti ambaye alikuwa akifanya kazi za ndani, ambao hawakuwapo wakati tukio hilo likitokea.

Mwendesha mashitaka huyo alidai kuwa kitendo hicho cha mauaji ni kinyume cha kifungu cha 196 na 197 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyorejewa mwaka 2002.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji isipokuwa kwa kibali maalum.

Hakimu Lukuna aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 17, mwaka huu, itakapotajwa tena hivyo mshtakiwa alipelekwa mahabusu kwa kuwa kosa hilo kisheria halina dhamana.

# Abambwa kwa tuhuma za kukutwa na meno ya tembo

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

POLISI mkoani Katavi wanamshikilia mkazi wa Kijiji cha Songambele wilayani Tanganyika kwa tuhuma za kukutwa na meno manne ya tembo na kipande kimoja akiwa ameyapakia kwenye baiskeli yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa katavi, Benjamin Kuzaga, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa juzi majira ya saa 2.30 usiku.

Alisema askari polisi walipata taarifa kuwa mtuhumiwa huyo anajihusisha na biashara haramu ya nyara za serikali ambazo alikuwa anazipata kinyume cha sheria ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Baada ya taarifa hizo, alisema polisi walianza kuandaa mtego kwa lengo la kumnasa na hatimaye kumnasa akiwa na meno mazima manne na kipande kimoja.

Alisema nyara hizo zilikuwa amezibeba ndani ya mfuko aina ya salfeti akiwa amepakia kwenye baiskeli yake yenye namba S7 G 20138 katika barabara ya Mpanda kuelekea Ikola. Kwa mujibu wa Kuzaga, mtuhumiwa huyo bado anaendelea kushikiliwa na polisi na upelelezi utakapokamilika, atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Kamanda Kuzaga alisema katika tukio lingine, Masoud Mbaruku (60), mkazi wa Kijiji cha Ruhafe wilaya ya Tanganyika, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa na silaha aina ya gobore yenye namba 424 kwenye mtutu akiwa anamiliki bila kibali.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na gobore hilo juzi majira ya saa 9 alasiri akiwa amelificha ndani ya kambi ya muda ya uwindaji haramu ndani ya hifadhi ya msitu wa Tongwe Mashariki.

Kamanda huyo pia alisema polisi wamewakamatwa watu wawili katika maeneo tofauti ya wilaya za Mpanda na Mlele wakiwa na dawa za kulevya aina ya bangi.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Jegi Lubinza (42) mkazi wa Kijiji cha Kabunde wilaya ya Mlele akiwa na bangi kete 16 na gramu 25 akiwa amezificha ndani ya nyumba yake na nyingine akiwa ameichimbia ardhini kwenye salfeti.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine aliyekamatwa kuwa ni Joseph Erick (37) mkazi wa Kata ya Itenka, Mpanda aliyekamatwa akiwa na bangi kete mbili. Alikamatwa kwenye eneo la Katente ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi akiwa amehifadhi ndani ya mfuko wa suruali yake kwenye kipande cha gazeti.

Alisema kuwa watuhumiwa hao wote wanatarajiwa kufikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma zinazowakabili.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi James Kilaba, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Jumuiya ya Mawasiliano ya Nchi za Afrika Mashariki (EACO), jijini Mwanza jana. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Hasunga, kigogo wa mbolea wateta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Topic ya Cairo nchini Misri, Mhandisi Raouf Bakry jijini Dar es Salaam.

Katika kikao kazi kilichofanyika Ofisi za Wizara ya Kilimo, Mhandisi Raouf, alimweleza Hasunga kuwa lengo la ziara yake ni kuangalia uwezekano wa kutumia fursa ya mkopo nafuu inayotolewa na Benki ya Exim ili kufanya biashara kati ya nchi za Afrika.

Alisema akipatiwa mkopo huo, ataongeza uwezekano wa kusambaza mbolea na viuatilifu ili kuongeza tija na kasi ya uzalishaji wa mazao mbalimbali ya wakulima.

Hasunga kwa upande wake alimweleza Raouf kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli, imedhamiria kutekeleza kwa vitendo azma ya maendeleo ya viwanda, hivyo inawakaribisha wawekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo viwanda vya kusindika mazao.

Alisema Rais Magufuli amejipambanua katika kuimarisha uwezekano wa wawekezaji kuwa na uwekezaji uliotukuka ili kuwanufaisha Watanzania sambamba na manufaa yao wenyewe.

Mkutano huo baina ya Waziri Hasunga Mhandisi Raouf, ulihudhuriwa pia na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mbolea ya Taifa (TFC), Salum Mkumba.

# HABARI KITAIFA



Mfanyabiashara ndogo ndogo akiwashawishi abiria walioko kwenye magari kununua visu katika Barabara ya Nelson Mandela, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni kinyume na agizo la Jeshi la Polisi la kuzuia uuzwaji holela wa silaha mbalimbali. **PICHA: JOHN BADI**

## Utegemezi wahisani sasa asilimia nane

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema kiwango cha utegemezi kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo katika bajeti kimepungua kutoka asilimia 12.5 mwaka 2017/18 hadi asilimia nane 2019/20.

Sambamba na hilo, amesema serikali itaendelea kuzingatia ombi la viongozi wa kidini kutafuta suluhu ya mambo mbalimbali ya maendeleo bila kuathiri Katiba ya nchi.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipomwakilisha Rais John Magufuli kwenye Mkutano wa Halmashauri Kuu ya 53 ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) ulioambatana na hafla ya kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa kitegauchumi cha jumuiya hiyo, jijini hapa.

Alisema serikali imeendelea kupunguza kiwango cha utegemezi kwa kuwa ndio msingi wa uongozi wa Rais Magufuli wa kujenga uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Kuimarika huko kwa bajeti yetu kunakwenda sambamba na kuimarika kwa huduma za kijamii kama vile elimu, maji na kupungua kwa umaskini na mahitaji muhimu."alisema

Waziri Mkuu alipongeza CCT kwa kuanza kuchukua hatua za kujenga uwezo wa ndani wa kujitegemea kiuchumi kwa kuwa zinahitajika nguvu za pamoja katika kuhakikisha wanawahudumia Watanzania na kuwaletea maendeleo.

"Kujizatiti kwa CCT katika kufikia malengo yake ya kujitegemea kiuchumi ni muhimu katika kutimiza kusudio na agizo la Mungu la kuwahudumia wahitaji ambao ni Watanzania lakini pia mtakuwa mnajaliza juhudi za Serikali katika wajibu wake wa kuwahudumia wananchi,"alisema.

Majaliwa aliwataka viongozi wa dini waendelee kuimarisha malezi na mafundisho ya kiroho kwa vijana na kuepusha mmomonyoko wa maadili ili Taifa liendelee kung'ara, kuheshimika na kusifika duniani kwa utulivu, amani na umoja.

Alisema serikali inatambua mchango wa madhehebu ya dini ikiwemo CCT katika kutengeneza mustakabali mwema na ustawi wa familia kupitia mahubiri ya injili na malezi ya kiroho kwa waamini.

"Tunatambua mchango wa malezi ya kiroho katika ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla na mafundisho yake kwani

INAENDELEA UK. 8

## Utetezi mauaji ya mke Julai 8

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji, imepanga kusikiliza utetezi wa Yusuph Musa anayekabiliwa na kesi ya madai ya kumuua mke wake, Fatuma Mbaga kwa makusudi, Julai 8 mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Pamela Mazengo, baada ya upande wa Jamhuri kuita mashahidi wanane na kufunga ushahidi wao.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali, Glory Mwenda.

Kabla ya uamuzi huo kusomwa shahidi wa nane, Koplo Thomas, alidai kuwa akiwa mpelelezi miongoni mwa vielelezo alivyokabidhiwa ni pamoja na ramani ya sehemu ya tukio.

Alidai kuwa kwa mujibu wa ramani aliyokabidhiwa, Fatuma aliuawa na mshtakiwa ndani ya chumba chake nyumbani kwake.

Shahidi huyo alikabidhi ramani hiyo mahakamani na ilipokewa kama kielelezo katika kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri ulifunga ushahidi wake na kesi iliahirishwa mpaka Julai 8, mwaka huu, mshtakiwa atakapoanza kujitetea.

Kwa mujibu wa wakili wa mshtakiwa huyo, Agustino Kusarika, Musa atajitetea binafsi na hatakuwa na shahidi.

Katika kesi ya msingi, Musa anadaiwa kuwa Mei 11 ,2015 eneo la Jangwani, Ilala, Dar es Salaam, alimuua kwa makusudi mke wake, Fatuma Mbaga.

## Biteko awapa mtihani wachimbaji wadogo

**Na Mohab Dominick,** SHINYANGA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amekabidhi leseni kwa vikundi 23 vya wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu wa Mwakitolyo wilayani Shinyanga huku akiwataka kufuata sheria na masharti ya uchimbaji .

Wananchi waliokabidhiwa leseni hizo ni wale waliokuwa wakichimba dhahabu katika eneo la Nyaligongo, Kata ya Mwakitolyo. Eneo hilo lilikuwa likimilikiwa na mgodi wa Acacia zamani Barrick.

Waziri Biteko alikabidhi leseni hizo juzi kwa wachimbaji hao alipofanya ziara ya kikazi kwa lengo la kutekeleza agizo la ugawaji wa leseni za uchimbaji lililotolewa na Rais John Magufuli.

Alisema kuwa kufuatia kupatikana kwa leseni hizo na kuelekezwa kupitia mafunzo waliyopatiwa wachimbaji wote wahakikishe kila baada ya mwezi mmoja wanawasilisha taarifa ya uzalishaji kwa mujibu wa kifungu cha 101 cha Sheria ya Madini ya 2010 na marekebisho yake ya 2017 na kifungu cha 16(1) cha kanuni za Madini cha mwaka 2018.

Aliwaagiza wachimbaji hao kuhakikisha wanafuata masharti ya leseni zao ikiwa ni pamoja na kulipa malipo ya Mrabaha unaotokana na uzalishaji wa Madini katika leseni zao kwa mujibu wa kifungu cha 87 cha sheria ya Madini 2010 na marekebisho yake 2017, pamoja na kifungu cha 90 (a)3 cha sheria ya fedha cha mwaka 2001 na marekebisho yake mwaka 2017.

Aidha, Waziri Biteko alisema kazi ya serikali kupitia Wizara ya Madini ni kuwalea wachimbaji wadogo ili kukua na kuondokana na uchimbaji mdogo na kuongeza kuwa haiwezekani watu kutoka Congo na Msumbiji walete madini yao kwenye masoko ya Tanzania.

"Mchukieni mtu anayetorosha madini. Mkimuona toeni taarifa, nafurahi pale Watanzania wengi wanatoa taarifa za mtu anayetorosha madini, vile vile kila mtu awe mlinzi wa mwenzake. Ninyi mpo mnaosha kwa kutumia mekyuri hata tajiri nae muulizeni umeuza lini? umeuza wapi?. Akikufukuza kwa kuhoji nitumie ujumbe nitashughulika naye," alisema.

Pia Waziri huyo aliwaeleza kuwa mgodi huo kabla ya kupewa leseni hizo, haukuwa na tija yoyote ile na ni miaka mitatu sasa na rekodi

INAENDELEA UK. 8




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi mashindano CHAN yasiwe zimamoto

**SOKA** ni moja ya mchezo ambao unachezwa kwa kalenda inayozunguka, ambapo wadau na familia ya mchezo huo unaopendwa zaidi duniani huita msimu.

Kumalizika kwa msimu mmoja, ni mwanzo wa maandalizi ya msimu unaofuata, iwe ni wa mashindano ya ngazi ya wilaya, kitaifa au kimataifa.

Wakati kiuhalisia, msimu au kalenda ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), bado inaendelea huko nchini Misri, timu ya Tanzania maarufu Taifa Stars yenyewe imeshatolewa katika mashindano hayo.

Fainali hizo sasa zimeingia katika hatua ya 16 Bora, na katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), ni timu moja tu ambayo ni Uganda (The Cranes), ndiyo ilifanikiwa kutinga hatua hiyo. Vigogo hao wa Cecafa, jana usiku walikuwa wakivaana na wenyeji, Misri na endapo watafanikiwa kusonga mbele, watakuwa wamejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi, baada ya kufanya vibaya katika fainali mbili zilizopita.

Tukirudi hapa nyumbani, Taifa Stars imesharejea nchini na sasa inatakiwa kujiandaa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambapo nchi zitakazokuwa zimefuzu, zitachuana hapo mwakani.

Taifa Stars ambayo haitakuwa na nyota wake wanaocheza soka la kulipwa katika nchi mbalimbali hapa ulimwenguni, akiwamo nahodha, Mbwana Samatta, ambaye anaichezea KRC Genk ya Ubelgiji. Katika kampeni ya kuwania tiketi ya mashindano hayo, Taifa Stars ambayo iko chini ya Kocha Mkuu Mnigeria Emmanuel Amunike, imepangwa kuanza na Sudan, na itaanzia nyumbani huku mchezo wa marudiano ukitarajiwa kuchezwa mjini Khartoum.

Ili Taifa Stars iweze kupeperusha vema bendera ya Tanzania, zinahitajika juhudi za kweli katika kuwandaa wachezaji wa timu hiyo kimwili na kifikra. Hii inatokana na wachezaji hao kutoka kusikia maneno ya kukatishwa tamaa baada ya kupata matokeo mabaya katika mechi za Afcon.

Wachezaji wa Taifa Stars wanatakiwa kupewa muda unaofaa kujiandaa na mchezo huo wa kwanza dhidi ya Sudan, lakini pia wakizingatia muda wa kupumzika baada ya kumaliza msimu uliopita. Benchi la ufundi linatakiwa kutoa programu zake ambazo zitasaidia kuwainua wachezaji hao, katika kupambana kuwania nafasi hiyo muhimu.

Nipashe inaamini kwamba, kalenda ya mashindano haya haikuwa kwa kushtukiza, TFF na Idara yake ya Ufundi, iliyafahamu na sasa wanachotakiwa kukifanya ni kuendeleza pale walipoanza kabla ya kikosi kamili kwenda Misri kushiriki Afcon. Gazeti hili linapenda kuwakumbusha wadau kwamba, soka ni mchezo wenye matokeo ya aina tatu ambayo ni kushinda, kutoka sare au kufungwa kama mnacheza mechi za ligi, au kushinda pamoja na kushindwa kwenye michezo ya mtoano.

Hivyo basi, pamoja na maandalizi yote hayo, ni lazima tukubali kuwa sisi ni wanamichezo, pale tunaposhuhudia timu yetu imepoteza mchezo, na mpinzani akisonga mbele.

Ni vema kwa kila mmoja kukubali kuheshimu matokeo na vile vile kukubali mapendekezo ambayo yanatolewa na walimu wa timu husika, kwa sababu mwisho wa siku, Nipashe inaamini kwamba hakuna kocha ambaye anapenda kuona kikosi chake kinafungwa kwa sababu, matokeo hayo huhatarisha ajira yake.

Naamini kupata nafasi ya kushiriki Fainali za CHAN, kutatoa fursa nyingine kwa wachezaji wa Tanzania kutangaza vipaji vyao kwa mawakala mbalimbali kutoka ndani na nje ya bara la Afrika. Tayari, Taifa Stars imekaa miaka 11, tangu iliposhiriki kwa mara ya kwanza Fainali za CHAN mwaka 2008, tunaamini safari hii itapambana ili kurejea mapema na si kusubiri hadi miaka 39 kama ilivyorejea kwa mara nyingine kwenye Fainali za Afcon.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tikiti ni moto wa kwanza

Na Barnabas Maro

**TIKITI** huiva vizuri kutokana na moto wa kwanza. Methali hii hutumiwa kutunasihi kwamba tuyatakapo mambo yetu yafanikiwe lazima tuyashughulikie mapema bila ya kupoteza wakati.

Ni dhahiri kuwa timu zetu za kandanda nchini zimekuwa kama watu wanaosindikiza wengine kwenye mafanikio kisha wasindikizaji kurejea nyumbani mikono mitupu. Hufanywa kama 'viwanja' vya kufanyia mazoezi na wachezaji wetu huwa watalii! Kwa ufupi timu haziandaliwi ipasavyo.

Nalilaumu Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuruhusu vilabu vyetu kusajili wachezaji 10 kutoka nje ya Tanzania. Kwa maana hiyo, timu zaruhusiwa kusajili wachezaji 10 wazawa na 10 kutoka nnje ya nchi. Kwa utaratibu wa mchezo wa kandanda duniani, wachezaji wanaocheza uwanjani ni 11. Kwa hiyo timu ikipanga wachezaji nane wa kigeni, waliobaki ni watatu tu wazawa!

Wahenga walisema "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho. Methali hii yatufunza tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine. Pia yatukumbusha kuvithamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama vya watu wengine.

Ni kweli kuwa wachezaji wetu wengi hawakidhi haja ya vilabu vyetu ndo sababu ya TFF kuruhusu usajili wa wachezaji 10 wageni ili kunogesha mchezo wa kandanda nchini. Matokeo ya ruhusa hiyo kumeifanya Tanzania kutokuwa na wachezaji mahiri wanaoweza kupambana kwenye michezo ya kimataifa na kuiletea Tanzania sifa.

Kama wachezaji 10 wanaosajiliwa kutoka nje watakuwa bora zaidi kuliko wetu, ni dhahiri timu za nyumbani zitakuwa dhaifu kiasi cha kushindwa kupambana na timu ngeni na hivyo kuzifanya hata timu za taifa kuwa dhaifu. Inapokuwa hivyo, mchezo wa kandanda unapoteza hamu ya kuutazama na matokeo yake ni idadi ya watazamaji kupungua viwanjani!

"Usijivunie cha mwenzako." Maana yake usijivunie kitu ambacho si chako. Hutumiwa kutukumbusha kuwa hatupaswi kuvionea fahari vitu visivyokuwa vyetu; tuvionee fahari vitu vyetu wenyewe.

Wachezaji wanaosajiliwa kutoka nje, tena kwa gharama kubwa kuliko wachezaji wetu, yatokeapo mashindano makubwa, huenda makwao kuzipa nguvu timu zao za taifa na kutuacha na wachezaji wetu wasiokuwa na uzoefu wala uhodari wa kucheza na timu za nje.

Mara ya mwisho Tanzania kushiriki mashindano ya Afrika ilikuwa miaka 39 iliyopita timu ikiwa na Watanzania watupu bila mchezaji hata mmoja kutoka nnje. Kwa nini? Kwa sababu wakati ule hakukuwa na utaratibu wa kusajili wachezaji kutoka nchi za nnje.

Tatizo letu ni kuwa na maneno mengi kuliko vitendo. TFF inaridhika na hali hii? Nionavyo, jibu la swali hili ni 'NDIO!' Kwa nini? Kwa sababu hakuna juhudi zinazofanywa na TFF kuwa na timu bora kama za wenzetu. Kwa mfano, ukubwa wa maeneo ya nchi za Burundi na Rwanda ni kama baadhi ya mikoa yetu kwa ukubwa.

TFF hailioni jambo hili? Au macho yao yanaziangalia Simba na Yanga tu? Zimefanya nini mpaka sasa? Mara ya mwisho timu hizo kutwaa Kombe la Kagame ni mwaka gani? Kwetu sisi kusherehekea Simba kufikia hatua ya pili kuelekea fainali ya Kombe la Afrika (ingawa ilitolewa), twaisifu utadhani imetwaa Kombe!

Je, Simba ingetwaa Kombe ingekuwaje? TFF ingejinasibu kuwa imeisaidia Simba? Kwa lipi hasa? TFF haistahiki sifa kwani ilipofikia Simba ni juhudi za viongozi wake wala TFF haina cha kujivunia. Hakuna juhudi zozote muhimu zilizofanywa na zinazofanywa na TFF kuzinufaisha vilabu vyetu zaidi ya kuwa "Domo kaya samli kwa mwenye ng'ombe."

Katika moja ya makala zangu za michezo kuna wakati nilipendekeza kutumia muda huo kujenga timu za taifa (Taifa Stars, Serengeti Boys, Ngorongoro Heroes n.k.)

Timu hizo zitajengwaje? TFF iwe na shule maalum ya mchezo wa kandanda itakayokuwa na walimu wenye utaalamu wa kutoka nchi za nje. Baada ya hapo iunde timu ya walimu (makocha) wa kandanda watakaozunguka nchi nzima kuchagua wachezaji vijana kutoka timu mbalimbali za mikoani. Wote wawekwe kwenye shule maalum itakayowapa maarifa ya mchezo huo.

"Ukipanda upepo, utavuna tufani (dhoruba)." Maana yake ukipanda upepo utaishia kuvuna kimbunga. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayepuuza mashauri anayopewa na kuishia kupatwa na matatizo mengi sana. TFF zindukeni. Au bado mpo usingizini?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Chai bora yajigamba kuzalisha bidhaa bora

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Chai Bora, imesema inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuzalisha bidhaa zenye viwango vya kimataifa zikiwamo za majani ya chai, kahawa na dabaga.

Katika kuhakikisha inakuza uchumi wa taifa na Watanzania kwa ujumla, kampuni hiyo imesema imeajiri vijana wa Kitanzania wanaozalisha kilo milioni 3.5 kwa mwaka.

Meneja Masoko wa Chai Bora, Awatif Bushiri, akizungumzia uzalishaji wa bidhaa hizo zenye ubora jana, alisema wameendelea kushiriki maonyesho ya biashara kimataifa kwa lengo la kuwaonyesha Watanzania namna wanavyozalisha bidhaa zenye ubora.

"Chai Bora ni wachanganyaji na wapakiaji wa aina za chai zinazokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ndani na nje ya nchi na tumeajiri Watazania wengi katika kuhakikisha tunakuza uchumi wa taifa," alisema.

"Tuna furaha kukaribisha Watanzania katika banda letu ili waonje bidhaa zetu. Katika jitihada za kuunga mkono kilimo, chai zetu zinatengenezwa kutokana na malighafi bora zinazozalishwa nchini na pia tunachangia katika kutengeneza fursa za ajira."

Alisema wanatumia malighafi bora za Kitanzania na ubunifu wa hali ya juu na kupitia ubunifu huo wanafurahi kuwa washindi wa kwanza katika kipengele cha banda bora la bidhaa za chakula na vinywaji katika maonyesho hayo.

"Iwe ni majani ya kawaida au yale yaliyo katika vipakti vidogo, wateja wetu wanaweza kufurahia bidhaa zetu zikiwa katika mfumo wowote wanaopendelea," alisema Awatif.

Chai Bora pia huuza bidhaa zao nje ya nchi katika nchi za Kenya, Afrika Kusini, Nchi za Falme za Kiarabu, Rwanda na Ghana.

# Amwaga chozi ushahidi kesi ya mauaji ya mkewe

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA John Thomas (59), jana alimwaga machozi na kwikwi wakati akitoa ushahidi katika kesi ya mauaji ya mke wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Katika ushahidi wake, alidai kuwa msichana wake wa kazi, Oriana Hamisi, alitoroka nyumbani kwake baada ya mauaji ya mke wake mdogo Silvester Paul siku 23 baada ya kuajiriwa.

Kadhalika amedai kuwa kabla ya kutoroka alimpulizia mtoto wake mchanga dawa ya kuuwa wadudu yenye jina la IT.

Thomas alitoa ushahidi huo huku akishikwa na kwikwi ya kulia jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji chini ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Pamela Mazengo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Grace Mwanga na Chesenci Gabiola.

Shahidi huyo alidai kuwa makazi yake ni Vingungutu Kiembembuzi, jijini Dar es Salaam.

Alidai Machi 27, 2014 alikuwa akiishi eneo mtaa wa Miembeni akiwa na familia ya wake wawili, mkubwa Manju Thomas na Silvester (kwa sasa marehemu), watoto wao watatu na msichana wa kazi, Oriana, ambaye alianza kazi Machi 4, mwaka huo.

Alidai kuwa siku hiyo, nusu ya familia iliondoka asubuhi, mke mkubwa aliondoka saa 12:00 na yeye na watoto wawili wanaosoma waliondoka saa 12:30 asubuhi huku wakimwacha mke mdogo na mtoto wake mchanga wa mwaka mmoja na nusu na msichana wa kazi.

"Saa saba mchana niliongea na mke wangu mdogo nikiwa kazini, Kunduchi, lakini ipofika saa 11:00 jioni nilipigiwa simu na aliyekuwa dereva wangu kwamba mtoto amerudi shuleni amegonga geti muda mrefu nimpigie simu mama mdogo amfungulie," alidai kuhu akimwaga machozi na kwikwi kwa kilio.

"Nilimpigia simu mke wangu mdogo hakupokea, nikamjulisha dereva wangu amvushe mtoto ukutani ili akajue ndani kuna nini. Nilipigiwa nikaambiwa kuna tukio kubwa ikanilazimu nirudi nyumbani, nikamkuta mke wangu amelala kwenye dimbwi la damu na ana jeraha juu ya sikio la kushoto. Nilimbeba kumuwahisha hospitalini lakini tuchelewa alishapoteza damu nyingi alifariki dunia" alidai na kuangua kilio.

Alidai kuwa mwili ulihifadhiwa katika chumba cha maiti na aliporejea nyumbani alikuta sebuleni kumetapakaa damu nyingi na shoka likiwa chini limejaa damu.

Alidai kuwa wakiwa pamoja na polisi waliingia chumbani kwa mke mdogo kulikuwa kumevurugika kabatini nguo zote ziko chini, dhahabu zimeibwa, kamera ya video na simu ya mke wake pia havikujulikana vilipo.

Walipomtafuta msichana, majirani walieleza kwamba walimwona akiondoka na bodaboda huku akiwa na mzigo.

"Nikaanza kumtafuta mtoto wangu mchanga tulimkuta amelala ananuka dawa ya kuuwa wadudu naona alitaka kumwua na mtoto wangu," alidai Thomas huku akilia.

Alidai kuwa walilazimika kwenda kwa Dada Amina aliyemletea msichana huyo anaishi Tabata Segerea lakini hawakufanikiwa kumkuta naye alishatoroka wakalazimika kwenda kumkamata mume wake na bibi yake ndipo akajisalimisha polisi.

Hata hivyo, alidai kuwa Amina alipoulizwa kuhusu mahali alipo msichana alikana kufahamu lakini baada ya siku sita kumalizika shughuli za mazishi, Oriana alimpigia simu akidai amepata ajali yuko Tabata lakini tayari kitengo cha mawasiliano cha jeshi la polisi kilinasa mawasiliano hayo na kubaini yuko jijini Arusha.

Baada ya wiki mbili, alidai kuwa walifanikiwa kumkamata Arusha akiwa anafanya kazi kwa mtu mwingine kwa kushirikia na askari polisi waArusha na Dar es Salaam.

Alidai kuwa walipompekuwa walikuta na kamera, simu ya marehemu, kadi ya ATM ya benki ya KCB, funguo sita,mkoba na cheti cha hospitali cha mtoto wa marehemu.

Shahidi aliomba mahakama ivipokee kama kielelezo katika kesi hiyo na mahakama ilikubali.

Katika kesi ya msingi, Oriana anadaiwa kuwa Machi 27,2014 alimuua kwa makusudi Silvester kwa kumpiga na shoka kichwani.




Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Fimbo Butallah (kulia), akielezea ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kampuni hiyo, kwa mmoja wa wateja Erasius Rweikiza (katikati), katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahifadhi waonywa kupiga wafugaji

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

SERIKALI imezipiga marufuku hifadhi za wanyamapori nchini kuwapiga wafugaji na kupiga mnada mifugo yao pindi wanapowakamata wakiwa wameingia ndani ya hifadhi badala yake wawapeleke kwenye vyombo vya sheria.

Onyo hilo limetolewa jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega, alipokuwa akizungumza na wafugaji wa wilaya ya Tanganyika katika ukumbi wa Idara ya Maji mkoani Katavi, mjini hapa.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi wa mamlaka zinazohusika na uhifadhi wa misitu na wanyamapori kuwapiga wafugaji na kuwatoza faini, kisha kupiga minada mifugo yao pindi wanapokamata mifugo bila hata kuwapa nafasi ya kujitetea.

Ulega alisema mamlaka hizo zinapaswa kutambua kuwa sheria za haki za wanyama zipo ila wao wamekuwa wakiangalia zaidi sheria zinazohusu kuingiza wanyama ndani ya hifadhi.

Pia alisema wafugaji nao wanapaswa kuacha kuvunja sheria za nchi na watendaji nao wasiwaonee pia waache migogoro baina yao na wakulima kwa wao wizara hawako tayari kuona wafugaji wanavunja sheria kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Alisema Rais John Magufuli anataka mambo yawe sawa ndiyo maana aliagiza maeneo yote yaliyokosa sifa yaangaliwe na yatakayobainika watayaangalia ili kuwagawia wakulima na wafugaji.

Naibu Waziri alisema mapendekezo hayo ya maeneo yaliokosa sifa yalishapelekwa serikalini na wizara nane zimeshaanza kuyapitia mapendekezo kabla ya kuyatolea uamuzi wa kuyagawa.

Pia aliwaagiza wafugaji wote nchini kuhakikisha wanapeleka mifugo yao kwenye chanjo kwa kuwa suala la chanjo si hiari na mfugaji ambaye hataki kupeleka mifugo yake ni bora akaacha kufuga.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Saleh Mhando, alisema kumekuwapo suala la mifugo kukamatwa katika hifadhi za misitu na ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Alisema wafugaji wamekuwa na tatizo la kulishia mifugo pia ndani ya mita 60 kwenye kingo za mito na kwenye vyanzo vya maji kutokana na tabia ya kuwatuma watoto wao kuchunga mifugo hivyo kushindwa kuzingatia sheria hiyo.

# Magufuli, Kenyatta watema nyongo

INATOKA UK. 2

biashara pamoja na kuoana," aliongeza.

Pia alisema njia ya kumaliza ukabila na mipaka ni watu waoane ili mtoto akizaliwa asijue kama kwao ni Tanzania au Kenya bali mwana Afrika Mashariki.

"Nikiwa kiongozi wa Kenya ninasema kama kuna kitu ningependa kuona kabla wakati wangu kuisha ni sisi wana Afrika Mashariki tunakuwa kitu kimoja," Kenyatta alisisitiza.

Rais Kenyatta alisema wakati anashuka kwenye ndege, alimwambia ndugu yake (Rais Magufuli) kuwa yeye ndiye Rais wa kwanza wa nje kukanyaga Chato.

Naye Rais Magufuli alimpongeza Rais Kenyatta kwa hatua alizochukua kwa mtu mmoja ambaye alikuwa na lengo la kuwagawanya raia nchi hizo mbili huku akisisitiza kuwa nchi hizo zina uhusiano mzuri wa kihistoria ambao umekuwapo hata kabla ya ukoloni.

Alisema nchi hizo zinaunganishwa na Ziwa Victoria na Tanzania ina eneo kubwa zaidi wakati Kenya wao wana asilimia tano.

"Samaki wanaweza kutaga mayai Tanzania na kifaranga wakala Kisumu, Kenya. Mtu anaweza kusafiri kwa ziwa hili kutoka Chato hadi Kisumu, Kenya.

Pia alisema wananchi wa nchi hizo ni marafiki na ndugu ambao wanazungumza lugha moja na wana utamaduni unaofanana na Watanzania wengi Kenya ni nyumbani, vivyo hivyo kwa Wakenya kwa Tanzania.

"Sidhani kama kuna mkoa hakuna Wakenya, kuna wengine wana nyumba kubwa Kenya halafu nyumba ndogo ipo Tanzania," alisema Rais Magufuli.

Mbali na uhusiano wa wananchi, alisema pia serikali hizo zinashirikiana kupitia ushirikiano wa kibalozi.

"Mwaka 2009 tulianzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ya Tanzania na Kenya, tunashirikiana katika nyanja za kimataifa. Mara nyingi tumekuwa na kauli na misimamo ya aina moja," alisema.

Rais Magufuli alisema nchi hizo zimeweza kunufaika kiuchumi mathalani biashara ambapo mwaka jana zilikuwa na thamani Sh. trilioni 1.045 ambapo Tanzania iliuza Kenya bidhaa za Sh. bilioni 482.43 na kuagiza zenye thamani ya Sh. bilioni 565 kutoka nchini humo.

Pia alisema takwimu za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Kenya ni miongoni mwa nchi tano zinazoongoza kwa kuwekeza Tanzania ambayo ina miradi 504 yenye thamani Dola za kimarekani bilioni 1.7 ambayo imetoa ajira 50,929. Alisema ikilinganishwa na wawekezaji wa Tanzania walioko nchini humo, wamefungua kampuni 24 zenye thamani ya Dola za kimarekani bilioni 185.

"Wapo Watanzania na Wakenya wanaoshirikiana kwenye miradi mbalimbali ya pamoja, kwa mujibu wa Bodi ya Utalii ya Kenya mwaka jana, Watanzania 220,216 walitembelea nchi hiyo," alisema.

Rais Magufuli alisema nchi hizo, zimekuwa zikitekeleza kwa pamoja miradi ya maendeleo ikiwamo miundombinu ambapo tayari wamekamilisha barabara kutoka Arusha- Namanga hadi Kenya na kukamilisha vituo vya huduma mpakani. Alisema kwa sasa wanatekeleza mradi wa barabara kutoka Arusha, Horiri hadi Taveta pamoja na mradi wa kusafirisha umeme kwa nchi hizo.

Hata hivyo, Rais Magufuli alimweleza Rais Kenyatta kuwa ameweka historia kwa nchi kuwa ya kwanza kufika Chato na alimuhakikishia kuwa ujio wake ameufurahia.



Mtuhumiwa Oriana Hamis, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza na Polisi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusikiliza mashahidi wanne wa Jamhuri dhidi ya kesi inayomkabili ya mauaji ya Silvester Paul. **PICHA: HELLEN MWANGO**

# Waajiri wasiojisajili fidia waonywa

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi(WCF), umewaomba waajiri ambao bado hawajajisajili na mfuko huo kufanya hivyo ili kuwasaidia wafanyakazi wao kupata fidia wanapopatwa na matatizo kazini

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini wa WCF, Dk. Abdulssalam Omary, katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DTIF) yanayofanyika jijini Dar es Salaam

Dk. Omary alisema lengo la mfuko huo ni kushughulikia masuala ya fidia kwa wafanyakazi waliopo katika sekta rasmi ya umma na binafsi Tanzania Bara ambao hupata matatizo ya kuumia, kuugua au kufariki dunia kutokana na kazi wanazozifanya kwa mujibu wa mikataba yao.

Alisema asilimia 85 ya waajiri wakubwa wamejisajiri na mfuko huo, huku waajiri wadogo waliojisajiri wakiwa 75 na kwamba ni vyema kwa waajiri ambao hawajajisajili wakafanye hivyo haraka.

Alisema mfuko huo ni taasisi ya hifadhi ya jamii iliyoundwa kwa mujibu wa sheria kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 marejeo ya mwaka 2015 na kwamba kujisajili ni muhimu

"Mfanyakazi atakapoumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi, WCF utatoa huduma za matibabu, malipo ya ulemavu, malipo ya ulemavu wa kudumu, malipo ya anayehudumia mgonjwa, huduma za ukarabati na ushauri nasaha, msaada wa mazishi na malipo ya wategemezi," alisema.

Dk. Omary alisema tangu mwaka 2016 mpaka 2018, jumla ya Sh. bilioni sita zimelipwa kwa wafanyakazi waliopatwa na matatizo wakiwa kazini.

"Ninatoa wito pia kwa wafanyakazi kufuatilia kwa ajili ya kubaini kama waajiri wao wamejisajili na mfuko huu kwa sababu ni muhimu sana kwao, " alisema.

# Biteko awapa mtihani wachimbaji wadogo

INATOKA UK. 5

zinaonyesha kuwa kiwango cha kodi ni sifuri hali ambayo aliwapa mtihani wa kukusanya kodi baada ya kumilikishwa kihalali.

Naye Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum, alimweleza waziri kuwa wachimbaji walitii kauli ya Rais Magufuli ya kuwataka wasiondoke katika maeneo yao ya uchimbaji kutokana na agizo la ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kuwataka waondoke ili kumpisha mwekezaji mkubwa, kampuni ya Acacia anayedaiwa ndiye mmiliki wa eneo hilo.

Mwekezaji huyo anadaiwa alilishikilia kwa muda mrefu eneo hilo bila kuliendeleza hali iliyosababisha serikali kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo kuendelea na uchimbaji.

Mbunge huyo aliwataka wachimbaji hao kutumia fursa hiyo ya leseni za uchimbaji kufanya kazi kwa kujituma na kumuunga mkono Rais Magufuli kwa kulipa mirabaha ya serikali huku akiwasihi kutouza maeneo yao kwa kuwa serikali imeanza kuweka miundombinu muhimu kama elimu, barabara, umeme na maji.

# Utegemezi wahisani sasa asilimia nane

INATOKA UK. 5

yamesaidia kujenga watumishi wa umma ambao wamelelewa katika misingi bora ya kumcha Mwenyezi Mungu," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali inaamini kwamba watumishi wa namna hiyo watachapa kazi kwa bidii, uadilifu, uaminifu na kupiga vita vitendo vyote vya rushwa na ubadhilifu wa mali za umma.

Katika hafla ya uchangishaji fedha, Sh. milioni 357.35 zilipatikana na Waziri Mkuu alisema ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa CCT wa miaka mitano (2017 – 2022) wenye lengo la kuiwezesha CCT kujitegemea kwa kuwa na vitegauchumi vyake ambavyo vitaiwezesha kujiendesha kwa asilimia 80.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za CCT na madhehebu mengine ya dini katika kuwahudumia Watanzania kupitia sekta za elimu, maji, afya na shughuli za ujasiriamali.

Katibu Mkuu wa CCT, Mchungaji Canon Matonya, alisema jumuiya hiyo imeanzisha mkakati wa kuwa na vitega uchumi vyake kwa lengo kuondokana na utegemezi wa fedha za ufadhili ambazo zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka.

Alisema ili jengo hilo likamilike linahitaji Sh. bilioni 14.7.

# Usalama barabarani wajinadi kupunguza ajali

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

KITENGO cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi, kimesema kiwango cha ajali za barabarani kimeshuka kwa kasi, ukilinganisha na mwaka uliopita. Mafanikio hayo ni matokeo ya kampeni ya nyakuanyakua iliyoanzishwa kwa lengo la kupambana na ajali.

Taarifa hiyo ilitolewa jana mjini Babati na Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi Fortunatus Muslim, wakati akizungumza askari wa usalama barabarani mbele ya wanahabari.

Kamanda Muslim alisema ajali zimepungua kwa kiwango kikubwa, huku akitoa mfano kuwa mwaka 2017 Januari hadi Mei zilishuka kwa asilimia 33 wakati mwaka 2018 katika kipindi hicho zilipungua kwa asilimia 28.

Kupungua huko kunatokana na elimu inayotolewa kwa kushirikiana na wadau wa usafirishaji na usafi , kwa mujibu wa maelezo yake.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwataka polisi wa kikosi cha usalama barabarani, kutumia lugha nzuri kwa madereva na wadau wengine wa usafirishaji, ili kuepusha kupotea kwa mahusiano mema kati ya polisi na wateja wao wanaowapatia huduma.

Alisema lugha ambayo polisi wanaitumia inatakiwa kuwa nzuri kwa madereva, kwa kuwa hamna sababu ya kujenga uadui kati ya askari na dereva, maana dereva ni watu muhimu kwao na ndiyo wateja wao. Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani Mkoa wa Manyara, Mary Kipesha, akitoa taarifa ya hali ya usalama barabarani mkoani hapo, alisema, ajali zimepungua kwa asilimia 70 huku akieleza kuwa Januari hadi Mei mwaka huu, ni ajali mbili zilizotokea.

Alisema mafanikio hayo yametokana na juhudi mbalimbali za jeshi hilo na wadau wa usafiri na usafirishaji, hivyo wataendelea kushirikiana kudhibiti ajali za barabarani na kutekeleza maelekezo yote watakayopewa na viongozi wa ngazi za juu.

Kwa upande wake, dereva aliyezungumza na Nipashe Ally Salimu, alisema, hali ya usalama barabarani ni nzuri tofauti na zamani, maana kuna vidhibiti mwendo vya kutosha, madereva hawana nafasi ya kujiachia.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Jackson Sipitieck, akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani juzi, cha kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2017/2018, ambapo Halmashauri hiyo imepata hati safi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake wahimizwa kushiriki uchaguzi

**Na Zanura Mollel,**
LONGIDO

WANAWAKE wilayani Longido , Mkoa wa Arusha, wametakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, kwenye uchaguzi za serikali za mitaa, unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Musa Matoroka, alisema hayo wakati akizundua mashina nane ya wakereketwa wa Jumuiya ya Wanawake (UWT) katika Kata ya Longido.

Kata hiyo ni ngome ya Chadema wilayani humo. "Nawakumbusha mliopoteza kadi za kupigia kura au kuhama makazi na ambao hawajafikisha miaka 18 wakati wa uandiskishwaji na wanawake jitokezni kwa wingi kugombea nafasi za uongozi, alisema Matoroka.

Alisema wanawake wana uwezo wa kuongoza sawa na wanaume, hivyo ni vyema wakagombea nafasi mbalimbali za uongozi bila kuhofia mila na tamaduni za jamii ya kifugaji, ambazo ni kandamizi kwa wanawake.

"Wanawake mnaotoka jamii za kifugaji naomba mgombee nafasi hizi, ni muhimu sana na sisi tutawaunga mkono achaneni na dhana potofu kuwa wanaume peke yao, ndiyo wanaotakiwa kugombea nafasi hizi,"aliwaambia Matoroka.

Awali akimkaribisha Matoroka, Katibu wa CCM Wilaya ya Longido, Simba Gaddafi, alisema lengo la uzinduzi wa kampeni hiyo ya Longido ya kijani, ni kuhakikisha CCM inachukua mitaa yote ya wilaya hiyo, katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Tunaposema kampeni ya kijani siyo kuvaa nguo za kijani tuu kupeperusha benderа, azma yetu ni kuhakikisha CCM inashinda mitaa yote katika uchaguzi wa serikali za mitaa,"alisema.

Katibu wa UWT Wilaya ya Longido Judith Laizer, alisema, wanawake wa wilaya hiyo wamedhamiria kuhakikisha kuwa chama chao kinashinda, kutokana na serikali kuwaondolea kero mbalimbali ikiwamo ya maji na kuboresha huduma za afya.

"Tunaishukuru serikali kuona umuhimu wa kutuletea mradi mkubwa wa maji, kutoka wilaya ya Siha, wenye thamani zaidi ya Sh.bilioni 15 na ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao unaelekea kukamilika. Pia imetupa Sh.bilioni 1.5 na itatuongezea Sh.milioni 500 kwa ajili ya kuimalizia,"alisema Laizer.

# Wanaume wahimizwa kwenda na wenza kliniki

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAKAZI wa mji wa Babati mkoani Manyara wametakiwa kutunga sheria ndogo ndogo za kuwabana wanaume wanaokataa kuongozana na wake zao kliniki.

Wanaochenga kuwasindikiza wenza wao wameelezwa kuwa wanakosa elimu inayotolewa na wataalamu wa afya juu ya namna ya kulea mimba itakayoleta mtoto mwenye furaha.

Ushauri huo ulitolewa jana mjini Babati na Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Prisca Nyaki wakati akizungumza na Nipashe.

Katika mahojiano hayo alisema ushiriki wa wazazi wa kiume na wa kike kuhusu namna wanavyolea mtoto tangu akiwa tumboni ni suala lisilokwepeka.

Alisema kipindi cha ujauzito mwanamke anahitaji ushirikiano wa karibu kutoka kwa mumewe kama vile mwanamume kuwa karibu na mwenza na kumpa maneno ya faraja juu ya mtoto wao aliyeko tumboni.

"Mimi ninaona zikitungwa sheria ndogo ndogo kwenye vijiji za kuwabana wanaume wanaokataa kuwasindikiza wake zao kwenda kliniki wanapokuwa wajawazito itakuwa njia ya kuwafanya washiriki kikamilifu." Alisema Nyaki.

Alisema ni muhimu kwani wanapewa elimu ya kutunza mtoto wao tangu akiwa tumboni jambo ambalo litasaidia kuwapa faraja watoto wao na wake zao na kuongeza upendo kwa mama na mwana.

"Wanaume wakibadilika na kuwapenda wake zao, watoto nao watawapenda baba zao maana mtoto ambaye amependwa tangu akiwa tumboni na wazazi wake atakuwa na akili maana itakuwa imetulia,"alieleza.

Alisema wanaume wanaofika kliniki na wake zao wajawazito ni asilimia 57 na takribani asilimia 43 ya wanaume hawafiki kliniki kuwasindikiza wake zao.

Nyaki aliwashauri wanawake kufuata uzazi wa mpango pengine si vyema kuazaa watoto zaidi ya watano, ili kujiepusha na matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa kujifungua.


Alieleza kuwa kadri mama anavyozidi kuzaa mfuko wa kizazi unatanuka zaidi na anaweza kupata matatizo.

Anasema kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu wamepata vifo viwili vya kina mama vilivyotokana na uzazi.

Mkazi wa Singe, Shaban Musa, alipohojiwa kuhusu wanaume kukataa kuwasindikiza wake zao kliniki, alisema ni utamaduni waliourithi kutoka kwa wazazi wao maana zamani mambo hayo hayakuwapo.

Ni mambo mapya hivyo wataalamu wa afya na wadau wanatakiwa kutoa elimu ili jamii iweze kubadilika.

Mkazi mwingine wa Babati, Yohana Bura, alisema mwanamume kuongozana na mwanamke kwenda kliniki kupima mimba na kuangalia hali ya mtoto ni jambo jema ila kwa wale waliowapachika mimba wanawake ambao siyo wake zao ni ngumu maana wengi wanaogopa kufahamika.





# Wapata haki walizopokwa miaka 29

**Na Godfrey Mushi,** HAI

FAMILIA mbili zinazoishi katika wiaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, ambazo zilikuwa zikitaabika kwa miaka kadhaa kutafuta haki yao baada ya kupokwa mali na ndugu wa karibu, zimeeleza kufurahishwa na hatua ya serikali wilayani humo kuingilia kati na kufanikisha kurejeshwa mali zao.

Miongoni mwa familia zilizonufaika na mpango huo wa serikali wa kurejesha mali za wajane, yatima, familia masikini na wasiojiweza ni familia tofauti za Mariam Mbaga na Sara William.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliitisha mkutano wa wananchi wote kusikiliza, kujadili na kutatua kero zinazohusu mirathi.

Akizungumza muda mfupi baada ya mkuu huyo wa wilaya kuamuru mali walizopokwa na bibi yao mzaa baba kurejeshwa na kukabidhiwa mbele yake, mmoja wa waathirika hao, Mariam Mbaga alisema:

"Baba yangu (Mbaga), alifariki dunia mwaka 2000 na kuacha mjane na watoto wawili, na baada ya mazishi tukapokwa nyumba na mashamba aliyotuachia.

"Leo (jana) mimi nina miaka 27, lakini namshukuru Mungu tumepata haki yetu mbele ya Mkuu wa Wilaya. Baba yangu alikufa akaacha eneo la ardhi na bibi yangu akawa analisimamia lakini akauza upande mmoja na kujimilikisha mali zote. Nashukuru tumekabidhiwa eneo na nyumba aliyokuwa anaishi baba."

"Niliachwa mimi na mdogo wangu, mama yetu yuko hai, lakini alikuwa hawezi kupambania tupate haki yetu. Nilimwambia mama asikate tamaa iko siku Mungu atatusaidia tutapata haki yetu na leo (jana) amejitokeza DC (Mkuu wa Wilaya) na ametusaidia tumepata hiyo haki. Wenye matatizo kama haya wako wengi mitaani lakini si wote wanaofikiwa na taarifa za viongozi wanaotafuta kurejeshea watu haki zao."

Naye Sara William alisema yeye na ndugu zake wengine wawili wa kike wameteseka kwa muda mrefu kwa sababu tu baba yao mzazi aliamua kuwagawia mali sawa sawa na watoto wa kiume wa familia hiyo.

"Tumehangaika na mirathi hiyo mpaka mahakamani, barua zimeletwa za mahakama kuthibitisha uamuzi wa baba, lakini ndugu zetu wa kiume wanatusumbua. Sasa kwa mimi ndiye nimemwona mtetezi wetu, naamini mwafaka ndiyo umepatikana kufikia hapo.

Alisema baba yao aliita watoto wote akasema anataka awagawie mirathi, watoto wa kiume wakakataa, baba yao akalazimika kwenda ofisi ya kijiji kutoa taarifa na watoto wa kiume wakaitwa wakakataa, akaenda mahakamani na mahakama ikatoa ufafanuzi kwa barua rasmi kwamba mwenye uamuzi wa kugawa mali ni mwenye mali mwenyewe.

Kwa mujibu wa Sara, baada ya hapo, baba yao aligawa mashamba na viwanja, ng'ombe na mbuzi kwa watoto wote bila kugabua wa kike na wa kiume.

Alisema baada ya uamuzi huo wa baba yake, amekuwa halali kwa sababu ndugu yake mmoja wa kiume alishamjeruhi usiku kwa panga na alishawahi kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili jela kwa kosa hilo au kulipa faini ya Sh. 200, 000 akalipa na juzi, ndugu yake huyo huyo alirejea na kumwambia kwamba hatalima katika eneo hilo labda ahame.

Awali, Mkuu wa Wilaya hiyo (Ole Sabaya) wakati akizungumza na makundi ya wahanga wa mirathi wilayani humo, alisema wakibaini watu waliowaonea masikini au wajane na yatima kwa kupoka mali zao, Serikali yake nayo itatumia nguvu kuwanyang'anya vile vile.

"Tukiona wale walionyang'anya haki za watu kwa nguvu na sisi tutawanyang'anya kwa nguvu. Kama ulitumia short cut (njia ya mkato) kupata mali na sisi tutatumia 'short cut' kukunyang'anya hiyo haki yako ili tuondoe malalamiko,"alisisitiza Ole Sabaya

Alisema baadhi ya watu wakishajua wamedhulumu wengine, wanakimbilia mahakamani kuweka zuio la mahakama na kwa kuwa mahakama inafuata utaratibu wa kisheria, ndiyo sasa kimekuwa kichaka chao cha kwenda kudhulumia watu na kwamba hiyo ni laana na kwamba kuna baadhi ya viongozi wadini wanashiriki mambo ya ovyo kama hayo.



Mchuuzi wa ujilishe akiambaaambaa kando ya Barabara ya Mandela, wakati akisaka wateja, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# DC awawakia makandarasi

**Na Mary Mosha,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ameonya kuwa hatasita kuamuru kunyang'anywa kazi na kisha kufikishwa mahakamani mkandarasi yeyote atakayebainika kushiriki vitendo vya kuhujumu miradi ya umma ikiwamo ujenzi wa maabara ya kisasa ya kompyuta inayojengwa wilayani humo.

Senyamule alitoa tahadhari hiyo jana, baada ya kupokea msaada wa mifuko 100 ya saruji iliyotolewa na Benki ya TPB.

"Nataka niwaambie makandarasi na mafundi jamii mnaopewa zabuni za ujenzi wa miradi ya umma kama mradi wa ujenzi wa maabara ya kisasa ya kompyuta hapa Same. Kama mtajihusisha na hujuma kama vile kuiba vifaa vya ujenzi kama hii saruji hamtakuwa salama. Nitashughulika na nyie hadi mahakamani baada ya kuamuru kunyang'anywa kazi,"alionya Mkuu huyo wa Wilaya Kabla ya kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) wa TPB, Jema Msuya, alishauri kundi kubwa la vijana katika Wilaya ya Same kujikita katika mafunzo ya Tehama ili kuingia kunufaika kielimu na kuweza kukabiliana na soko la ajira.

Alisema kutokana na umuhimu wa vijana kupata mafunzo ya Tehama, benki yake iliamua kuwekeza katika jamii kwa kuhakikisha inapata elimu bora na yenye tija.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu anayesimamia ujenzi huo, Daniel Malonga, alisema msaada wa saruji walioupata utawasaidia kukamilisha ujenzi wa maabara hiyo itakayowasaidia vijana kuibadilisha wilaya kwa muda mfupi kutokana na mafunzo watakayopata.

# Mkuu wa Mkoa ataka uchimbaji chuma Same

**Na Mary Mosha,** HAI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amesema utajiri wa madini ya chuma ulioko katika Wilaya ya Same, unapaswa kuifikirisha upya serikali kuja na mpango mkakati wa kuyachimba kisasa ili kulinufaisha taifa.

Dk. Mghwira aliyasema hayo jana wilayani hapa wakati akimkaribisha Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, kuzungumza na menejimenti ya kiwanda cha kutengeneza vipuri cha Kilimanjaro Machine Tools Ltd (KMTC).

"Mkoa huu tumebahatika kuwa na utajiri wa chuma katika wilaya ya Same. Kama serikali itajielekeza katika uwekezaji wake, malighafi kwa ajili ya kuzalisha chuma nchini haitategemewa kutoka nje ya nchi, hivyo hakutakuwa na tatizo la malighafi kwa kiwanda cha kutengeneza vipuri cha Kilimanjaro.

Alisema kama kiwanda hicho kitaanza kuzalisha vipuri kama ambavyo Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) linakusudia ni wazi kuwa wachimbaji wa madini ya chuma katika wilaya ya Same watanufaika vya kutosha na jasho lao lakini pia serikali itanufaika na mapato yatokanayo na uchimbaji wa madini ya chuma.

Akizungumza na menejimenti ya kiwanda hicho, Waziri Bashungwa alisema wizara yake inaahidi kulifanyia kazi wazo hilo la Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro.

Waziri Bashungwa aliahidi kwamba kiwanda hicho cha kutengenezea vipuri kinafufuka haraka ili kuchochea uwekezaji wa migodi ya chuma ya Same na Liganga.

"Serikali inaangalia njia bora ya kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa tija ili kuleta manufaa mapana kwa wananchi wa eneo hilo na taifa kwa ujumla. Serikali inafahamu umuhimu wa mradi huu katika ujenzi wa uchumi, hatua za awali za ujenzi wa mradi zimekwishaanza kutekelezwa,"alisema Bashungwa.

Kuhusu masoko, Waziri Bashungwa alisema serikali inapambana kuhakikisha wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa wananufaika na masoko ya kimataifa.





Mkurungenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma, Dk. Semistatus Mashimba (kulia), akipokea moja ya kompyuta kutoka kwa Meneja Tathimini na Ufuatiliaji wa Taasisi ya Mkapa Foundation, Rahma Musoke, wakati taasisi hiyo ilipokabidhi msaada wa vifaa tiba, simu za mkononi 59 na kompyuta tano vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 80, wilayani humo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Baraza la wazee latoa kilio kwa serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BARAZA la wazee jijini Dodoma, limeiomba serikali kupitia upya sera ya wazee ya mwaka 2003 ili waweze kupata pensheni ya uzee ambayo itawapa nafasi ya kupata mikopo ili kuendeleza maisha yao.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee jijini hapa, Petro Mpolo, wakati wa uzinduzi wa baraza la kuchagua viongozi wa baraza hilo.

Mpolo alisema Serikali inapaswa kuwaangalia wazee kwa karibu hususan mikopo, ambayo hutolewa na halmashauri bila riba kwa lengo la kuwasaidia kuwainua kiuchumi.

Alisema mikopo isiyo na riba kwa wazee itawasaidia, kwa vile wanaweza kuitumia kuanzisha biashara, ambazo zitawasaidia kupata kipato cha kila siku.

"Tunaomba serikali itusaidie kupata mikopo inayotolewa na halmashauri kama wanavyopata vijana na akinamama, itatusaidia sana wazee," alisema Mpolo.

Mwenyekiti huyo alisema lengo lao ni kuona wazee wanapata nafasi kama yalivyo makundi mengine ambayo yanapata mikopo hiyo.

Kuhusu pensheni, alisema suala hilo kwa wazee linapaswa kuangaliwa ili waweze kujikimu kimaisha.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, alisema Serikali itaendelea kuwaenzi wazee kwa kuwa wana mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa, ikiwamo kutunza amani na utulivu iliopo nchini.

Katambi alisema serikali inatambua mchango wa wazee katika ujenzi wa taifa, ndio maana imekuwa ikiwajali kwa kila jambo ikiwamo kuwasikiliza. "Kundi la wazee ni muhimu sana, kwasababu linahitajika kusimamiwa ipasavyo ikiwamo kuwaheshimu," alisema Katambi. Aliwataka viongozi waliochaguliwa kuongoza baraza hilo kwa kuweka mbele maslahi ya wazee, ikiwa ni pamona na kuwasilisha hoja zao inapotakiwa ili changamoto zao ziweze kupata ufumbuzi.

Katika uchaguzi huo, Petro Mpolo alichaguliwa kuwa mwenyekiti na nafasi ya makamu mwenyekiti ilikwenda kwa Abraham Msuya, huku nafasi ya katibu ikichukuliwa na Mary Mchalo na Veronica Mveyekule alichaguliwa kuwa katibu msaidizi.

Wajumbe waliochaguliwa katika nafasi ya uwakilishi wa wazee kwenye baraza la madiwani ni Grene Simba na Gelard Lwiza,wakati nafasi ya mweka hazina imechukuliwa na Jonas Zitatu.

# RC: Tiba kituo cha Pwaga, ianze wiki ijayo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge,ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuhakikisha kuwa ifikapo Julai 15 mwaka huu, iwe imeanza kutoa huduma za afya katika kituo cha afya Pwaga.

Kituo hicho ni miongoni mwa vituo vitatu vilivyojengwa wilayani humo kupitia mpango wa kujenga na kukarabati vituo vya afya nchini.

Awali, wananchi eneo hilo walilazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya makao makuu ya wilaya na kituo cha Afya Kibakwe.

Akizungumza mara baada ya kukagua ujenzi wa kituo hicho, Dk.Mahenge alisema amejiridhisha ujenzi wa kituo hicho majengo yote yamekamilika.

"Vitu vilivyobaki ni vidogo vidogo sana, ambavyo vitarekebishwa kwa muda ambao tumekubaliana, umeme umeanza kuingizwa, maji yapo sasa ifikapo Julai 15, wananchi waanze kunufaika na matunda ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi huu," aliagiza.

Awali, mkuu wa wilaya hiyo, Jabir Shekimweri alisema majengo ya kituo hicho yamekamilika kwa asilimia 99 bado ufungaji wa umeme.

"Tayari nguzo zimeshafika na sasa kilichobaki ni kuingiza umeme ndani ya majengo,"alisema Shekimweri. Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wananchi walimshukuru Rais John Magufuli kwa kuwajengea kituo hicho kwa kuwa kitasaidia kuondokana na vifo vya mama na mtoto.

Zakayo Machali, alisema tayari kuna wauguzi na madaktari kwenye kituo hicho kwa ajili ya kutoa huduma za afya.

"Tulikuwa tunapata adha kwa kulazimika kwenda Mpwapwa. Kibakwe kwasasa huduma zitakuwa jirani na sisi," alisema Machali.

Alisema umbali waliokuwa wakiutumia kufuata huduma ya afya ulikuwa ukisababisha vifo vya akina mama na watoto.

# Vifo vya mama, mtoto vyapungua Chemba

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Chemba, Dk. Semistatus Mashimba amesema uwepo wa watoa huduma za afya ngazi ya jamii umepunguza idadi ya vifo vya mama na mtoto kwenye wilaya hiyo.

Dk.Mashimba alitoa kauli hiyo juzi katika makabidhiano ya vifaa tiba kwa ajili ya huduma za mama na mtoto katika zahanati ya Kelema wilayani humo vilivyotolewa na Taasisi ya Mkapa Fountation vyenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 80.

Alisema kuwapo kwa watoa huduma hizo kumechangia mwitikio mkubwa wa wananchi wengi kufika kupata huduma za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema taasisi hiyo ilianza kazi zake wilayani hapo mwaka 2018 ikilenga kuboresha huduma zinazotolewa vituo vya afya na ngazi ya jamii ikiwa imeajiri wahudumu wa afya 37.

Mkurugenzi huyo alisema wahudumu hao wamejengewa uwezo kupatiwa mafunzo, ambayo yameleta mafanikio ya afya katika ngazi ya kaya hadi wilaya.

Kwa upande wake Meneja Tathimini na Ufuatiliaji wa Taasisi hiyo, Rahma Musoke alisema taasisi hiyo imetoa vifaa tiba kwa baadhi ya zahanati za wilaya Chemba na kuwezesha mafunzo na vitendea kazi vyenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 80 kwa ajili ya huduma ya Mama na Mtoto katika wilaya hiyo.

Alivitaja baadhi ya vifaa hivyo walivyokabidhi kuwa ni simu za mkononi 56 zitakazotumika kwa ajili ya kukusanyia taarifa za kazi wanazofanya kila siku ili kuwasiliana na ngazi husika za huduma hiyo, na vifaa tiba vya huduma ya Mama na Mtoto.

"Pia tumetoa kompyuta za kupokelea taarifa na zitakazotumika kutoa elimu kwa wananchi wanaofika kupata huduma za afya kwenye zahanati kutokana kuwekewa programu maalumu ya masomo ya afya," alisema.


Alisema tangu kuanzishwa taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana na serikali kupitia Wizaya ya Afya ,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Menejimenti na Utumishi wa Umma kutekeleza miradi mbalimbali nchini.

Alizitaja zahanati zitakazonufaika na msaada huo katika wilaya ya Chemba kuwa ni Soya, Kelema, Mondo, Lahoda na Goima.

Aidha, alisema katika taasisi hiyo imetoa ajira kwa watumishi wa afya 37, ambao kati ya hao, wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni 35 na wataalamu wa afya wawili.

Alifafanua kuwa taasisi hiyo imetoa mafunzo katika ngazi ya jamii kuhusu majukumu yao ya kazi pamoja na kuwapatia vitendea kazi kama baiskeli, viatu, makoti ya mvua na mabegi ya kubebea vifaa vya kazi.

"Tumetoa mafunzo kwa wataalamu wa vituo 26 ili kuimarisha ubora wa huduma za upasuaji wa dharura kwa wajawazito," alisema.





# Atuhumiwa kutumikisha wasichana kingono

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linamshikilia mwanamama kwa tuhuma za kuwatumikisha kingono mabinti kutoka Tanzania Bara.

Aidha, Salome John (40), anadaiwa kuwachukua wasichana kutoka Tanzania Bara na kuwatumikisha kwenye biashara ya kuuza miili yao kwa wateja mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, alisema mtuhumiwa huyo ni mkazi wa Kizimkazi mkoa wa Kusini Unguja na wanaendelea kumuhoji kutokana na tuhuma zinazomkabili.

Alisema awali wasichana wanne ambao majina yao yanahifadhiwa walifika katika kituo cha Polisi Makunduchi kulalamika kuwa mama huyo, awali aliwaahidi kuwapa ajira katika baa yake, iliyopo huko Kizimkazi lakini ameshindwa kuwapa kazi hiyo na kuwataka wauze miili yao.

"Wasichana hao ambao wanatoka jijini Dar es Salaam walifika kituo cha polisi kulalamika baada ya kuona kuwa ni kinyume na makubaliano waliyokubaliana"alisema.

Mkurugenzi wa Wanawake na Watoto katika wizara yenye dhamana na wanawake na watoto, Nasima Haji Chumu, alisema walifanya mahojiano na wasichana hao ambao walieleza kuwa wapo Zanzibar kwa muda wa miezi mitatu na kwamba waliahidiwa na mtuhumiwa huyo kuja kufanya kazi za baa.

"Wasichana hao walieleza kuwa hawajalipwa mshahara wao kwa muda wa miezi mitatu wakati wakifanya kazi ya baa kwa mama huyo na walipomdai walimueleza kuwa wauze miili yao ili wapate fedha jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya kazi", alieleza.

Aidha, alivitaka vyombo vya dola kumchukulia hatua za kisheria mama huyo ili kudhibiti vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Mkoa wa Kusini Unguja, Idrisa Kitwana, ameagiza kuwa mama huyo aondoke katika kijiji hicho ili kuweza kuisuru jamii na vitendo viovu.

"Hatutaki kumuona kwa sababu akiendelea kukaa ataendelea kuwadhalilisha wanawake na hata kusababisha maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi,"alisema.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), akikabidhi cheti kwa mfanyabiashara bora, Hussein Njenje, wakati wa kongamano la wanachama wa klabu ya wafanyabiashara Mkoa wa Singida juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais akunwa na ubunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, amewapongeza vijana wazawa waliobuni mfumo mpya wa kurahisisha huduma za usafiri salama na uhakika unaozingatia wakati uitwao (Tan Tax).

Alisema ubunifu wao ambao unaungwa mkono na serikali utasaidia kutoa fursa za ajira ambazo kwa sasa ni changamoto kubwa kwa vijana wanaohitimu.

Balozi Iddi aliyasema hayo ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar wakati akizungumza na timu ya viongozi wa mfumo huo iliyofika kujitambulisha wakijiandaa kuuzindua rasmi siku chache zijazo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), muda wote imekuwa ikihimiza umuhimu wa ubunifu katika nyanja mbalimbali ndani ya jamii ambao hatma yake huleta faraja ya upatikanaji wa maendeleo sambamba na kupunguza au kuondoa changamoto zinazowazunguka watu.

Mkurugenzi Mkuu wa mfumo mpya wa kurahisisha huduma za usafiri salama na uhakika unaozingatia wakati, Salma Salum Othman, alisema lengo la kubuniwa kwa mfumo huo ni kusuluhisha usafiri ambapo Dereva atakayemhudumia abiria atakuwa katika njia salama.

Alisema dereva au abiria atakayeridhika na kukubali kupata huduma kupitia mfumo huo katika harakati zake za usafiri wa kila siku atajiunga kwenye mfumo husika kupitia simu yake ya mkononi baada ya kuwasilisha vielelezo vitakavyohitajika.

Mhandisi Mkuu wa Mfumo, Haji Masoud Abass, alieleza kwamba dereva ambaye atakuwa mwanachama atasajili bima yake,pamoja na leseni ili kuwekwa katika mfumo maalum atakaokuwa akiutumia katika kazi zake.

Haji alisema abiria mwanachama anapohitaji huduma za usafiri atatumia mfumo maalum kupitia simu yake ya mkononi itakayomuwezesha kupata huduma kwa usafiri na dereva atakayepangiwa.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi wa Mfumo , Abass Salum alieleza kwamba kutakuwa na ukurasa maalum katika njia ya mtandao wa mawasiliano katika kutoa taaluma kwa umma juu ya mfumo huo.

Abass alisema ukurasa huo utakwenda sambamba na upatikanaji wa matangazo ya mfumo huo kupitia njia za Face Book, Twiter, Whatsap na Instagram wakati watendaji na wataalamu wa mfumo huo wakiendelea kuutangaza kupitia Tv Online.

Alisema uzinduzi huo unatarajiwa kufanyika katika ukumbi wa taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni Zanzibar , Jumapili Julai 7, kwenye kilele cha Saba Saba ambayo ni Sikukuu ya Wakulima, kutakuwa na ofa ya Sh 15,000 itakayotolewa kwa kila dereva mpya ili kuhamasisha mpango huo.

Abass alisisitiza kwamba mfumo huo utazingatia gari kulingana na hadhi ya kila abiria na mtazamo wao wa baadaye kufikiria kuzitumia bajaji na bodaboda katika azma ya kurahisisha usafiri nchini.

# Wanawake waambiwa bila hati hakuna ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kuwaepusha wanawake wa Zanzibar na migogoro ya ardhi, Kamisheni ya Ardhi, imewataka kinamama kuhaulisha ardhi.

Ofisa Mwandamizi wa Kamisheni ya Ardhi Haji Mrisho, ametoa angalizo hilo, akiwataka wanawake kufanya uhaulishaji wa ardhi wanazomiliki ili kuepukana na migogoro inayoweza kujitokeza kwenye umiliki.

Akizungumza katika mkutano wa uhamasishaji wa uhaulishaji wa ardhi kwa wananchi wa kisiwa cha Uzi ng'ambwa, alisema wanawake wengi wamekuwa wakidhulumiwa ardhi kutokana na kutokua na hatimiliki.

Aliwataka wananchi wa kisiwa hicho hasa wanawake kutokubali kuuziwa au kugawiwa ardhi bila kuwa na vielelezo muhimu.

Alisema iwapo watakuwa na nyaraka za hatimiliki za umiliki wa ardhi hakuna atakae dhulumu au kuwanyang'anya rasilimali hiyo.

Asha Ramadhan Bakari, mkaazi wa kijiji hicho aliwashauri wanawake wenzake kuacha kutoa fedha zao kuwapa wanaume kwa ajili ya ujenzi au ununuaji wa vitu vya thamani.

Alisema kuwa wanawake wamekua wakinyanyasika hasa pale ndoa inapovunjika bila ya kuthaminiwa mchango walioutoa kujenga na kuanzisha familia.

Kwa upande wake Mwanasheria wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar Fatma Kwale, alieleza kuwa Tamwa imekua ikitoa elimu ya umiliki wa ardhi kwa wanawake baada ya kugundua kuwa wanawake wengi Zanzibar wamekuwa wakidhulumiwa katika masuala ya umiliki wa mali. "Tunaimani kuwa elimu hii tunayoitoa sasa tunaamini kuwa wanawake watakuwa na uelewa wa kusajili mali zao ikiwamo ardhi hata kama ardhi walionayo wamepewa zawadi kutoka kwa waume zao au wazazi wao,"alisema.

Aliwataka wanawake wa kisiwa hicho kutofumbia macho vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanavyofanyiwa wanawake na watoto kwani kuendelea kuwalinda wahalifu wa vitendo hivyo ni kulea udhalilishaji.

Mkutano huo wa uhamasishaji wa umiliki wa ardhi umeandaliwa na Tamwa Ofisi ya Zanzibar, kupitia mradi wake wa 'pazaa' ili kuwajengea uwezo wanawake katika kumiliki ardhi na rasilimali muhimu kwa maendeleo.



**YEMI ALADE AVUNJA REKODI YOU TUBE**

Soma UK.20

JUMAMOSI JULAI 6, 2019

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# WEMA..WEMA..LOH! Wakili azidi kupasua ukweli

## BASI SAWA



## Alfredy afuta 'Machozi' kwa albamu

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili nchini, Alfredy Benedict Funda, amesema amekamilisha albamu mbili 'Futa Machozi' na 'Kusudi ' kwa mwaka huu pekee.

Mwimbaji huyo wa wimbo 'Mungu wa Zawadi' amesema yupo mbioni kukamilisha nyimbo zingine ili kutoa albamu ya tatu.

"Lengo langu ni kuinua imani za watu na kuwavuta watu kwenda kwa Mungu, kwani tukiwa na hofu tunaweza kufika mbali na jamii yetu ikaishi kwa amani,"alisema Funda.



## Walimbwende K'ndoni waingia kambini

SHINDANO la Miss Kinondoni Dar es Salam, limeanza rasmi kwa washiriki 18 kuingia kambini kwa ajili ya kufanya mazoezi.

Akizungumza na BT, mwandaaji wa shindano hilo, Nancy Kikwembe alisema washiriki hao wamejichimbia hapo watajifunza mambo mbalimbali ikiwamo ubunifu, Mchujo wa kuingia hatua ya awali ilifanyika wiki mbili zilizopita ni sasa tumeingia kambini," amesema.



# Dogo janja amkoga Irene Uwoya kwa 'Kishada'

BAADA ya mwanamuziki wa Bongofleva, Dogo Janja, kuachia ngoma mpya 'Kishada' mitandao ya kijamii imechafuka baada ya baadhi ya watu kudai ni dongo kwa Irene Uwoya.

Wimbo huo ambao Dogo Janja amemuimba kwa kumsifu mrembo mmoja, umeleta utata baada ya sehemu ya shairi kueleza anataka afanane naye licha kuna watu wanabisha.

Kwa siku ya tatu pekee wimbo huo umetazamwa na watu Zaidi ya 100,000 huku katika baadhi ya ujumbe unasema ni ujumbe tosha kwa aliyekuwa mkewe Irene ambaye ameonekana kula raha kivyake.

## INSTA-TWITTER





**Hawa** jamaa wa bodaboda akikubeba anakuongelesha hata husikiii kwa sababu ya upepo. Sasa unabaki 'eee ndiyo, ndiyo eee', Unaweza kujikuta unakubali kuolewa bure. 'Nikupeleke gheto?' 'eee ndiyo'.- **Roma Mkatoliki.**



**Wakenya** kila kitu chetu wanataka. Wameenda 'half time' wakasikia Watanzania tumepigwa magoli 3-0 wakaona wivu. 'Na sisi tunataka.'- **Idriss Sultan.**

UNASEMAAA...

# Miss Kilimanjaro watembelea yatima

WASHIRIKI wa Shindano la kumsaka Mlimbwende wa Mkoa wa Kilimanjaro mwaka huu, wameshiriki kazi mbalimbali za kijamii ikiwamo kutembelea watoto yatima.

Akizungumza na BT, Mkurugenzi wa taasisi ya Dees Bridal and Entertainment ambao ndio waandaaji wa Shindano hilo, Dotto Olafsen amesema hatua hiyo ni kutambua umuhimu wa mtoto wa kike kusaidia jamii inayowazunguka.

"Washiriki licha ya kutambua umuhimu wa kusaidia jamii mathalan, kwa sasa taasisi yangu iko katika kampeni maalumu ya kutokemeza mimba za utotoni hasa kwa wanafunzi kupitia sanaa na burudani mbalimbali katika wilaya ya Hai" anafafanua Mkurugenzi huyo.





# Finally atambulisha 'Mukide' redioni

MSANII wa muziki wa Bongofleva , Finally, amesema wimbo wake mpya uitwao 'Mukide' utaanza kurushwa leo katika vituo vya redio na televisheni.

Finally ametamba ngoma hiyo kali inatokana na kazi ya Studio mpya ya Pilipili Music Manra ikiwa ni lebo inayohusisha uibuaji na uendelezaji wa vipaji kwa wasanii chipukizi .

"Najisikia furaha kubwa kwani singo hii mpya itachochea mafanikio katika muziki wangu baada ya Januari mwaka huu kuweza kuachia singo yangu ya kwanza iliyoitwa 'Go down'," Alisema Finally.

BODA 2 BODA

# Mambo TvSwahili yamuenzi Kanumba



CHANEL mpya ya kuonyesha filamu za Bongo MamboTvSwahili imeanza kupeperusha kazi za wasanii chipukizi.

Mmoja wa wasanii Rahmu Davidi amesema wasanii chipukizi wamefurahia kuonekana katika chanel hiyo na kuwafanya kazi zao kujulikana.

"Filamu zingine za wasanii wakubwa kama This Is It ya Kanumba zinaoneshwa katika MamboTvSwahili, kama kichocheo cha watu kutazama zaidi," alisema msanii huyo.




>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Sio** kila umpendae basi unaweza mbadilisha. Mwingine anaweza kukupenda na bado akawa hayupo tayari kubadilika. Mtu wa kumbadilisha mtu huyo ni yeye mwenyewe. Kwa hiyo hapo mawili, uachane naye au uendelee kuwapo na kuvumilia kasoro hizo - **Hamisa Mobeto.**



**Kwa** moyo wa Unyenyekevu mkubwa mimi na mke wangu tunasema asante kwa wote ambao kwa namna moja au nyingine kwenye kutimiza ndoa yetu, kuanzia ibada pale mbezi mpaka sherehe pale Mlimani City kama kwa nama yoyote ulitusaidia tunasema Asante Mungu akubariki - **MC Pilipili.**



**Natamani** kuzaa. Loh! Wakuzaa naye sasa!!! - **Amber Lulu.**

# Kuumbe!



## WEMA..WEMA..LOH! Wakili azidi kupasua ukweli

SAKATA la kuachiwa na kukamatwa tena kwa nyota wa filamu nchini, Wema sepetu, limeingia sura mpya baada ya wakili wake Albet Msando, kudai polisi walikiuka utaratibu wa kisheria kumkamata tena msanii huyo.

Akizungumza na redio EFM jana, Msando amesema kisheria mteja wake hakupaswa kusumbuliwa na polisi hao kutumia nguvu kumkamata kama vile amefanya uhalifu.

Alisema kisheria polisi wangemtaarifu mteja wake sababu ya kumkamata tena, na si kutumia nguvu kama ilivyoonekana juzi katika mahakama ya mkazi ya Kisutu.

Tukio hilo lilitokea dakika chache baada ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde, kutamka Wema yuko huru, na kuzikubali hoja za upande wa utetezi kwa kutumia kifungu cha 225(5) cha mwenendo wa mashtaka ya makosa ya jinai.

"Tukio lile lilifanyika kinyume na taratibu, polisi wanatakiwa kamkamata mtu lazima wamtaarifu kwa kumtajia kosa lake, lakini si kutumia nguvu kama ilivyokuwa kwa Wema na ndio maana Waziri wa mambo ya Ndani, Kangi Lugora anakemea suala hili," amesema Msando.

WAFURAHI KUACHIWA HURU

Baadhi ya wasanii, ndugu na marafiki wa Wema Sepetu, wamefurahia kitendo cha kunusurika kulala mahabusu kwa mara nyingine, baada ya kupewa dhamana na Kituo Kikuu cha Polisi

Katika mitandao ya kijamii baadhi ya mashabiki wake wamemsifu Msando kufanya kazi kubwa kumuokoa mrembo huyo kulala mahabusu.

Wema ambaye aliwahi kushika taji la Miss Tanzania mwaka 2006 anakabiliwa na mashtaka ya kurekodi video ya ngono na kuisambaza katika mitandao ya kijamii.







COSMAS

## Vijembe 'kuntu' kwenye muziki wa dansi

Na Adam Fungamwango

USIDHANI ni taarabu tu ndiyo kuna nyimbo za kupigana vijembe na mafumbo, hata kwenye muziki wa dansi zipo.

Kwa sasa kwenye bongo fleva naona kumepungua nyimbo za kupigana vijembe, badala yake asilimia zaidi ya 90 ni mapenzi kwa kwenda mbele.

Hata muziki wa dansi wa kisasa nao unaonekana kupunguza sana nyimbo za kuimba na kutupiana madongo, lakini taarabu huwa haiishi kwa sababu ndiyo asili yake.

Leo tunawaletea baadhi ya nyimbo za dansi ambazo zilikuwa ni vijembe kwenda kwenye bendi nyingine au mwanamuziki waliomkusudia.

Pamoja na hayo, uzuri wa nyimbo hizo zilikuwa hazitaji mtu jina wala aliyekusudiwa, ila muhusika atakuwa amepata ujumbe.

### RADHI YA WAZAZI-JUWATA JAZZ BAND


Wimbo huu ulitungwa na kiongozi na mpiga solo wa bendi ya Juwata Jazz, Msondo Ngoma, Said Mabera, mwanzoni mwa miaka ya '80. Dhana ya wimbo huu ni kwamba Mabera alimuimba mwanamuziki mmoja aliyehama kwenye bendi hiyo na kwenda bendi nyingine hasimu.

Inasemekana kuwa mwanamuziki huyo alikuwa anaishi kwa wakwe zake. Kwa hasira ya kuhama, Maber alimtungia wimbo huo aliokuwa na baadhi ya maneno haya. 'Wakwe zako wamenifuata, kunilalamikia unawabana humu ndani. Kati ya wewe na mkeo nani kaolewa, wamechoka kulisha mke na mume.'

### POLE MZEE-DDC MLIMANI PARK

Hayati Shaaban Dede ni mmoja wa watunzi wazuri wa nyimbo na vijembe. Wakati akiwa Sikinde katikati ya miaka ya '80 alitunga wimbo uitwao 'Pole Mzee.' Ni kibao ambacho inadaiwa aliitungia bendi yake ya zamani wa Msondo Ngoma. Wachungzi wa masuala ya muziki wanasema kuwa alikuwa akiwakejeli kuhusu wanamuziki wengi wa bendi hiyo kuhamahama na kwenda bendi zingine.

'Watoto wamekimbia nyumbani umebaki na wajukuu pia watasambaa. Iliyobaki nitamuuliza shemeji una kasoro gani hapo nyumbani. Jirekebishe na hao waliosalia wasiondoke. Pole mzee.' Ni baadhi ya maneno ya vijembe kwenye wimbo huo.



DEDE

### MV MAPENZI NO 2-MLIMANI PARK

Ni wimbo uliotungwa mara tu baadhi ya wanamuziki wa Sikinde walipohama kwenda kujiunga na Orchestra Safari Sound (OSS) na kuasisi mtindo wa Ndekule. Awali kulikuwa na wimbo wa MV Mapenzi, lakini ukatungwa namba mbili yake katikati ya miaka ya '80. Maudhui ya wimbo huu moja kwa moja ulionekana kuwalenga walioihama bendi hiyo wakiongozwa na Muhidini Maalim Gurumo.

'Kuchafuka kwa bahari siyo mwisho wa safari. Meli ilipokumbwa na dhoruba nahodha kajitosa baharini. Wale papa na nyangumi wenye uchu wamemmeza.'

Walikuwa na maana kuwa Gurumo ambaye alikuwa kiongozi wa Sikinde ndiye nahodha aliyejitosa baharini, pamoja na mabaharia wengine ambao ni wanamuziki.



MABERA

### CHATU MKALI-OSS

Wimbo huu ni kama jibu la wimbo wa 'Mv Mapenzi'. Ulikuwa ni utunzi wa Bitchuka mwaka 1985, ambaye alikuwa mmoja wa waliohama kutoka Sikinde.

Baada ya wimbo wa Sikinde na wao walitunga kibao cha kuujibu wimbo huo, wakitoa onyo kali kwa wanaomchezea chatu. Pamoja na kwamba ni kijembe, lakini ulitungwa kwa staili ya lugha ya picha.

'Usimchezee Chatu, dongo usimtupie utaukosa ushindi. Natoa onyo kwa yoyote anayechezea chatu, atakuwa asipate lolote la manufaa na ajali imkute bila ya kutegema, atakuja aadhirike ajute na dunia.'

### MTOTO AKILILIA WEMBE-MLIMANI PARK

Butchuka, akiwa OSS alitunga kibao cha 'Homa Imenizidia' Dhana ya wimbo huo ni kama vile alichoshwa na maisha ya kule aliko. Lakini aliimba kama mwanamke aliyedanganywa na kumuacha mumewe kwenda kuolewa na mtu mwingine, lakini asipate kile alichoahidiwa.

Sikinde, bendi ambayo alikuwa ametoka kwenda OSS, inatunga wimbo ulioonekana kama kuujibu wimbo wake. Ulitungwa na Cosmas Chidumule ambaye kwa sasa ameokoka.

'Mtoto akililia wembe mwache umkate, akatapopata kidonda ndipo atakapouogopa. Ndugu yetu tulikuasa kwamba yule bwana mdanganyifu, ukasema akakujengea nyumba, atakununulia gari, sasa unajuta kwa sababu hakuna cha gari wala kibanda ulichoambulia.'

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Njia mbaya inapogeuka peponi

**Na Adam Fungamwango**

NI mipango ya Mwenyezi Mungu tu. Siku zote kazi ya Mungu huwa haina makosa. Kwenye maisha binadamu anaweza kuwa amepitia katika mazingira magumu, mabovu na hata ambayo ni machafu kwenye jamii, lakini baadaye yakamfikisha kwenye neema, au mafanikio.

Na baada ya hapo kwa binadamu inabaki ni stori na kumbukumbu kwenye maisha yake, lakini akiwa hawezi tena kufanya vile kwa sababu ilikuwa ni mapitio tu, na kwa kiasi kikubwa ni mipango ya Mungu kumfikisha pale alipo.

Ifuatilie kwa makini filamu ya 'Mungu Nisitiri' inayoonyesha jinsi baadhi ya binadamu wanapopita kwenye mitihani migumu.

Imechezwa na mastaa wengi tu, kila Bi. Hindu, Hemed Suleiman, Baba Haji, Asha Bui, Asia Datchi, Shamira Ndwangira, maarifu kama Bi. Staa na wengineo.

Aisha Bui aliyecheza kama mama Salha, alikuwa amekaa mlangoni mwa nyumba yake. Mara binti yake pekee mdogo akarejea kutoka shule. Akamweleza kuwa anadaiwa fedha za chakula, maji na ulinzi shuleni. Mama akaanza kutoka kwa machozi, mtoto asijue kwa nini mama yake analia.

Aisha anakwenda kwa wifi zake, Bi Hindu na Bi. Staa kuomba msaada wa kumsaidia na mtoto wake, lakini wanamtimua.

Akiwa hajui hili wala lile Salha, anakwenda kucheza na wenzake, lakini manyanyaso anayoyapata kwa kupigwa mara kwa mara, huku akisimangwa kuwa hana baba wala mtu wa kumtetea, linamfanya Salha kumuuliza mama yake alipo baba yake. Hatimaye mama anaamua kumueleza ukweli.

Hemed na mkewe Aisha hawaelewani kutokana na tabia mbaya ya mwanamume. Kazi ni kumpiga mkewe na kumnyanyasa. Mke anaamua kwenda kwa mganga.

Anaporejea anamkuta mumewe amerejea na kumuuliza alikuwa wapi. Mke alimuongopea mumewe, jibu ambalo lilimfanya Hemed kumpiga mkewe kwa hasira.

Akakimbia nyumbani kuepuka kipigo. Aliporejea alimkuta mumewe amesomba vitu vyote vya ndani na kutoweka, huku kodi ya nyumba ikikaribia kwisha. Wakati huo Aisha alikuwa na mimba changa.

Alikaa peke yake, lakini hali ikawa ngumu akaenda kwa wifi zake, ambao hawakuwa msaada kwake, kwani nao walikataa kuwa mimba si ya kaka yao, hivyo akawa anahangaika. Baadhi ya majirani walimpa hifadhi hapo alipojifungua mtoto akamwita Salha. Akaanza kufanya biashara ndogo ndogo ili kumudu kumtunza mtoto wake, lakini hali iliendelea kuwa ngumu. Hapo ndipo Salha alipogundua kuwa baba yake alimkimbia. Akaendelea maisha ya mama yake.

Maisha yaliendelea kuwa magumu kiasi cha mama kuamua kujiingiza sasa kwenye biashara ya ukahaba.

Siku moja alipata mteja ambaye alimlipa pesa nyingi zaidi kuliko kawaida. Lakini jamaa huyo akamwambia kuwa yeye alihitaji kumuoa ili aachane na biashara hiyo na kuwa mke mwema na mwanamke anayejiheshimu.

Aisha akamwambia anafanya kazi ile kutokana na ugumu wa maisha na si vinginevyo.

Mtu yule ni Baba Haji ambaye alifunga ndoa na na Aisha, wakaishi raha mustarehe na mtoto wao Salha ambaye sasa alifurahi kumpata baba mwingine.



BAHATI YAKE

# Rapa anusurika kuuawa Marekani

WANAMUZIKI wa Hip hop nchini Marekani, Slim 400, amenusurika kuuawa baada ya kufyatuliwa risasi na watu wasiofahamika.

Kulingana na chanzo cha uhakika, Slim alikutwa na tukio hilo usiku wa Jumatatu ya wiki hii wakati akiendesha gari, ndipo alipotokea mtu aliyevaa kofia iliyoziba sura na kumtishia risasi kwa lengo la kumuua.

Wakati huo Slim alikuwa akiongea na simu na pembeni yake alikaa rafiki yake kibiashara Mud Dollaz.

Amesema nyota huyo wa muziki kabla ya tukio hilo alikuwa eneo hilo akimsubiri Mud kwa muda mrefu katika studio moja ya kurekodi muziki.

Wakiwa katika hali ya utulivu, ghafla rapa huyo alisikika akipiga kelele "oh shit."

Baada ya hapo, chanzo hicho kilisema kwamba Dollaz alionekana kushtushwa na mtu huyo, kisha sauti ya kike iliskika ikiwataka kuinamisha vichwa vyao chini kwa kuwa wanalengwa kwa bunduki.

Katika kile kinachoaminika kiliweza kumuokoa rapa huyo dhidi ya kifo ni gari kuwa na uwezo wa kuzia risasi.

Lakini walifanikiwa kusimama haraka na kuruka haraka ndani ya gari zaidi ya mita 400 kabla muuaji huyo hajawafikia tena.

Hata hivyo risasi hizo ziliharibu gari yake karibu na dirisha ambalo yeye alikuwa amekaa.



# Yemi Alade avunja rekodi You Tube

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Yemi Alade, amezidi kung'ara baada ya kuwa msanii pekee wa kike aliyetimiza wafuasi milioni 100 katika mtandao wa You tube.

Msanii huyo mwenye kipaji cha kuimba amefanikiwa kuvunja rekodi hiyo kutokana na kibao chake cha Johnny ambacho kilitazamwa na idadi hiyo ya watu duniani kote.

Aidha watu milioni moja wamerekodiwa kuikubali video yake iliyowekwa katika chanel yake.



## Elisha ona unavyowatoa povu watu

BAADHI ya mastaa nchini Nigeria, wameungana kupinga kitendo cha Mbunge wa Seneta Elisha Abbo, kumpiga makofi mwanamke mmoja ndani ya duka la wanasesere.

Abbo (41) kutoka jimbo la Adamawa alitembelea duka hilo akiwa na watu wengine , lakini alipoingia ndani alikosana na mmoja wa wauzaji wa duka hilo na ndipo alipoanza kumpiga hadharani jambo ambalo wengi hawakulifurahia.

Mara video fupi ya tukio hilo kusambaa mtandaoni, wasanii kama Don Jazzy, Toke Makinwa na MI Abaga walisema kitendo hicho hakikubaliki kufanywa na kiongozi kama yeye na anatakiwa kuomba radhi wanigeria.

## Big Brother Nigeria yaanza kwa ngumi

MSIMU wa shindano la Big Brother Nigeria, umefunguliwa na washiriki wameanza kutimua vumbi ndani ya nyumba wakiwania kitita kikubwa cha fedha.

Lakini washiriki wakiwa na siku tano tu ndani ya jumba hilo, tayari mambo yamekuwa moto kwa baadhi ya washiriki baada ya Tacha na Thelma nusura wapigane baada ya kutuhumiana kuharibu chakula.

Washiriki hao walisikika wakitupiana maneno makali na kutaka kushikana kwa nia ya kuchapana ngumi, lakini huku wenzao walijitokeza kuwatenganisha.





## Ubakaji wamchefua Stella Damasus

MKALI wa filamu kutoka Nollywood, Stella Damasus, amevunja ukimya baada ya kuelezea namna rafiki yake alivyobakwa na mchungaji wa kanisa moja.

Damasus amesema rafiki yake huyo alikabiliwa na msongo wa mawazo kutokana na vitisho kutoka kwa mchungaji huyo Fatoyinbo.

Matukio ya kubakwa yanaendelea kujadiliwa katika mitandao ya kijamii nchini Nigeria, baada Busola Dakolo kuelezea tukio la aina hiyo.

## CDQ awaogopa vijana wa SARS

MWANAMUZIKI aliyejizolea umaarufu nchini Nigeria, CDQ, ameeleza jinsi alivyonusurika kupigwa risasi na kikosi kinachoogopwa mchini humo cha kuzuia uporaji kinachojulikana kama SARS.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliandika kwamba Julai 2, 2019, alipatwa na tukio hilo baada ya askari hao kumlenga kwa risasi yeye na marafiki zake waliokuwa pamoja.

Lilikuwa jambo la kutisha na lenye kusumbua wakati askari hao walipotuvamia na kutulenga kwa bunduki mimi na rafiki zangu," amesema CDQ.





## Mionzi ya Sheria

# Sheria haijawaacha matapeli wa mapenzi

Na John Juma
0716217615

YAMKINI ulikuwa au bado upo katika uhusiano na mwanamume au mwanamke, ambaye mmefikia ngazi ya uchumba. Ulimpatia au unampatia zawadi nyingi naye anakupa au unampatia zawadi kulingana na hali zenu kiuchumi.

Na zaidi sana mnajiwekea ahadi ya kufunga ndoa kwa msingi huo, mmoja wenu mume au mwanamke unajitoa sana kumhudumia, kumjali kwa matarajio kuwa karibuni mnakuwa mke na mume.

Lakini, cha ajabu, katika mazingira usiyoyaelewa mambo hayaendi si kama ilivyokuwa awali.

Kwa lugha nyepesi hakuna upendo wala mapenzi motomoto. Au kama bado yapo, kwa huyo mwenzako ni kama danganya toto, anacheza na akili na hisia zako.

Ni dhahiri, shahir hana malengo na wewe tena wala hakumbuki siku za nyuma umemgharamia sana, kuanzia fedha, mali na muda.

Sasa unaanza kujiuliza hivi haiwezekani kurejeshewa tena au kufidiwa vitu hivyo?

Majibu ya maswali haya yote ni ndiyo. Ni ndiyo, na gharama pamoja nazo zawadi zinaweza kurejeshwa. Sheria imeongelea hata mambo ya uchumba, ndiyo ukweli.

Wengi tunaijua sheria katika kuongelea wizi, dhamana, mikataba, mirathi au ndoa, lakini ni vyema tukajua kuwa sheria ni pana na imeongelea mambo mengi mno. Hili la uchumba nalo ni sehemu ya yaliyofanyiwa kazi.

**KUDAI FIDIA**

Kifungu cha 69,(1) (a)-(b) Sura ya 29 ya Sheria ya mwaka 1971 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010, kinaelekeza, mtu yeyote anaweza kufungua shauri mahakamani na kudai fidia baada ya uchumba kuvunjwa.

Kwa haraka haraka utakubaliana na mimi kuwa kwa mujibu wa tafsiri ya kifungu cha sheria hiyo siyo suala la kulazimisha au kushurutisha wahusika kuendelea na uchumba kama mmoja wao hataki kufanya hivyo, hasha.

Lengo kuu ni kumpoza mhusika aliyeumizwa kwa kumshurutisha mkosaji kulipa fidia kutokana na maumivu aliyoyapata msababishiwa. Tukiachana na suala la kurejesha zawadi.

Fidia inasimamia kama malipo kutokana na maumivu aliyosabishiwa mhusika, kutokana na 'matarajiohewa ya ndoa' sanjari na muda, fursa nyingine zilizopotezwa na tapeli huyo.

Na zawadi ni kurejesha kile ambacho tapeli alipokea. Isitoshe, masharti muhimu ya kuzingatia kabla ya kufungua shauri la madai ni kama vile, anayefungua lazima awe ndiyo aliyeumizwa, ahadi ya kuoana ilifikiwa au ilifanyika ndani ya mipaka ya Tanzania, siyo nchi nyingine na tena muda wahusika wanaanzisha mahusiano, wote wawili, tayari walishafikia miaka 18.

**KURUDISHA ZAWADI**

Kifungu cha 71 cha Sheria ya Ndoa Sura ya 29, mwaka 1971 kinatujuza kuwa mtu yeyote anayo haki ya kufungua shauri mahakamani kudai arejeshewe zawadi alizotoa kwa mtu ambaye, hapo awali kabla ya uchumba kukoma, alikuwa na ahadi ya kufunga naye ndoa na zawadi aliitoa kwa mlengwa na matarajio hayo.

Zawadi ni pamoja na fedha taslimu,hundi, nyumba, magari, nguo na kila kitu ambacho kina thamani- 'valuables'.

Hili ni bila ya kujali mali hiyo imeandikishwa, ipo kwa jina la nani, baina ya wahusika. Mantiki, ni mlalamikaji kumudu kuithibitishia mahakama kuwa kwa ridhaa yake ndiyo alimpatia mlalamikiwa mali husika kama zawadi.

Shauri la namna hii linaweza kufunguliwa katika ngazi yoyote ya mahakama iwe ya Mwanzo, Wilaya, Hakimu Mkazi au hata Mahakama Kuu. Kutegemea na thamani ya kiwango cha mali husika, ambazo zilipokelewa kama zawadi.

Mathalani, endapo zitakuwa zilikwishatumika kulingana na hali yake au hazipo tena, zimeuzwa au kutolewa zawadi kwa mtu mwingine. Zitatakiwa kulipwa kwa fedha taslimu,hundi inayolingana na thamani, bei ya soko wakati mlalamikaji alivyonunua au hata ikibidi kwa kununua nyingine kama hiyo, hizo ili kumrejeshea mdai.

Na ikishindikana kurejesha, mali binafsi za mlalamikiwa (tapeli), ambazo hata hazikuwa sehemu ya zawadi, zitauzwa ili kufidia deni.

Na ikitokea mhusika hana mali yoyote ya kuuza atatakiwa kwenda kutumikia kifungo, jela. Kwa muda ambao mahakama itaona inafaa, kama mfungwa wa madai.

Kwa mujibu wa kifungu cha 70 cha Sheria ya kesi inatakiwa kufunguliwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe hasa ya kuvunjwa huko kwa 'ahadi ya ndoa' kunako lalamikiwa.

**ANGALIZO**

Bilashaka kuanzia sasa tutakuwa makini sana katika kufanya maamuzi ya nani hasa inafaa kuanzisha naye uhusiano na kufika hatua ya uchumba.

Siku hizi masuala haya siyo mepesi tena, hata kidogo. Wazee wetu hawakupata kuifahamu kadhia hii ya 'matapeli wa kuchuma mali kwa kupitia mwanvuli wa mapenzi kwani nyakati zile hayakuwepo au walikuwa wachache sana.

Zama hizi ipo haja Watanzania vijana, wa kike na kiume kuwa macho zaidi kuchagua wenza kwa kipindi hiki ambacho pesa zimeshika hatamu ya sehemu kubwa ya maisha ya kila siku na huathiri mawazo, fikra, maamuzi na matendo ya binadamu karibu wote.



## Kalamu ya Mwalimu

# Ajali hizi zinatosha, tuchukue hatua sasa

Reubeni Lumbagala

AJALI ni moja ya majanga ya kijamii na kiuchumi ambayo hugharimu uhai wa Watanzania wengi wa kila rika.

Aidha, huharibu mali na miundombinu na kusababisha hasara kubwa kwani rasilimali nyingi hutumika kukabiliana nazo.

Ajali ambazo zimekuwa zikitokea zimesababisha vifo, ulemavu, uharibifu na upotevu wa mali za wananchi. Yapo makosa ambayo yanasababisha kutokea ajali barabarani.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Hamadi Yusuf Masauni, anayataja makosa yanayosababisha ajali barabarani wakati alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Manyinyi bungeni jijini Dodoma. Manyinyi alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuhakikisha tatizo la ajali linamalizika kutokana na kukithiri kwa ajali hasa kwa waendesha bodaboda na kuacha athari kubwa kwa jamii na taifa.

Naibu Waziri Masauni, alitaja makosa hayo kuwa ni pamoja na ya kibinadamu ambayo huchangia kwa asilimia 76, ubovu wa magari asilimia 16 na mazingira ya barabarani kwa asilimia nane.

Kalamu ya Mwalimu kama mdau mkubwa wa elimu ya usalama barabarani imeona ni vyema kupaza sauti yake katika janga hili la ajali za barabarani.

Kama taifa, wakati ni sasa wa kila Mtanzania kusimama katika nafasi yake na kupaza sauti dhidi ya uzembe ambao umekuwa ukisababisha ajali hizi. Makosa ya kibinadamu ndiyo yamechangia kwa asilimia kubwa ajali za barabarani. Hivyo basi, ni wakati wa kuhakikisha makosa haya ya kibinadamu ambayo yapo katika uwezo wa sisi wananchi kuyashughulikia kikamilifu ili kumaliza kabisa tatizo la ajali za barabarani na taifa kuelekeza jitihada zake katika kutatua changamoto nyingine zinazokabili nchi yetu.

Makosa ya kibinadamu yanajumuisha uendeshaji wa kizembe au hatari, ulevi, mwendo kasi, uzembe wa waendesha pikipiki wa watembea kwa miguu.

Dereva amepewa jukumu kubwa la kuhakikisha analinda uhai wake mwenyewe, uhai wa abiria na wa chombo cha moto anachokitumia katika safari yake. Hivyo, dereva awapo barabarani, anapaswa kukumbuka wajibu huu mkubwa ambao kama akiuzingatia ipasavyo, ajali zitapungua kwa asilimia kubwa.

Ni lazima dereva aendeshe chombo kwa umakini bila kusahau kuzingatia sheria na alama za barabarani. Mwendo wa chombo unapaswa kuwa wa wastani ili kuwa na uwezo wa kudhibiti chombo kuepuka kutokea madhara makubwa barabarani. Dereva hapaswi kunywa pombe pindi aendeshapo chombo chake.

Kutokana na wingi wa vyombo vya moto barabani, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani hushindwa kupima kiwango cha pombe kwa madereva wote.

Kutokana na changamoto hii, baadhi ya madereva wasio waaminifu huendelea kutumia pombe huku wakiwa safarini. Kila dereva ajichunge mwenyewe katika kuhakikisha hatumii kilevi cha aina yeyote awapo safarini kwani kutumia kilevi ni kuendelea kusababisha ajali ziongezeke katika jamii.

Abiria nao wanapaswa kuhakikisha wanapaza sauti zao dhidi ya madereva wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo mkali au wanaotumia kilevi. Namba za simu za maofisa wa usalama barabarani zipo katika magari. Abiria wawasiliane na viongozi hao pindi dereva akiwa mkaidi wa kuzingatia ushauri mzuri anaopewa na abiria wake wapenda usalama barabarani.

Watembea kwa miguu (pedestrians) nao wana jukumu la kutokomeza ajali kwa kuhakikisha wanazingatia sheria na alama za barabani pindi wanapotembea barabarani ili kutokuwa chanzo cha ajali. Watoto nao wasaidiwe kuvuka barabarani kwani wengi wao bado hawazijui sheria na alama za barabarani.

Chanzo kingine kikubwa cha ajali barabarani ni ubovu wa magari. Wamiliki wa magari watimize wajibu wao wa kuhakikisha magari yao yanakuwa katika hali bora kuwa na usafiri salama.

Magari yafanyiwe uchunguzi na kukarabatiwa (service) kubaini kama kuna ubovu wa aina yeyote ili tatizo au matatizo yatakayoibainiwa yaweze kufanyiwa matengenezo.

Wamiliki wa magari wawape nafasi mafundi magari kufanya kazi yao na kufanyia kazi ushauri watakaopewa na mafundi hao ili kuboresha magari yao.

Wamiliki hawapaswi kusubiri hadi tatizo litokee katika magari yao ndipo wayapeleke kwa mafundi. Hata pale gari litakapoonekana kwa nje kuwa lipo katika hali nzuri lipelekwe kwa mafundi kuchunguzwa ili tatizo litatuliwe mapema.

Magari yakiwa katika hali nzuri, ajali zitapungua, yapo mazingira ya barabarani ambayo nayo yanachangia kutokea kwa ajali.

Serikali itizimize wajibu wake wa kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara ili njia ziweze kupitika kikamilifu bila kusababisha ajali.

Tuseme yatosha kwa ajali hizi za barabarani, kila mwananchi ahakikishe hawi chanzo cha ajali bali mjumbe mwema wa kumaliza ajali. Ushirika wa pamoja unahitajika kati ya serikali, jeshi la polisi, madereva, wamiliki wa magari na wananchi kwa ujumla katika mapambano dhidi ya ajali za barabarani. Tanzania bila ajali, inawezekana, timiza wajibu wako .Tafakari.

**Maoni: (+255) 764 666349.**

MAKALA

# ‘Mila kandamizi chanzo watoto kujifungua watoto wenzao’

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TABIA ya wazazi na walezi mkoani Shinyanga ya kuendekeza mila na desturi kandamizi zilizopitwa na wakati, imeendelea kuwa na taathira kwa mabinti.

Hawa ndiyo wanaokatizwa masomo na kuozwa ndoa za utotoni ambazo matokeo yake ni ‘watoto kujifungua watoto wenzao.’

Mabinti ambao wamekuwa wakiozeshwa ndoa hizo za utotoni wana miaka 13 hadi 17 na wengi huachishwa masomo na wazazi au walezi wao kwa tamaa ya kupata mahari ya mifugo kuanzia ng’ombe 15 wakidhani wanaondoa umaskini kwenye familia zao.

Ndoa hizo huwaingiza watoto kwenye majukumu mazito ya kulea waume, kushika ujauzito na kujifungua watoto wenzao katika umri mdogo na baadhi yao hata viungo vya miili vikiwa bado kukomaa.

Matokeo yake ni baadhi kushindwa na ndoa na kuamua kutoroka kwenda mijini kutafuta maisha, baadhi wakiambuliwa kutumikishwa kazi za ndani ama kufanya biashara ya ngono katika umri mdogo.

Takwimu za kitaifa za mwaka (2012) zinaonyesha kuwa mkoa wa Shinyanga unaongoza Tanzania kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora 58, mkoa mwingine ni Mara 55 na kwamba mabinti hao huolewa wakiwa chini ya umri wa miaka 18.

Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga Nyanjura Mjuberi, anasema tatizo hilo la wazazi kuendekeza mila na desturi hizo zilizopitwa na wakati za kuozesha watoto wadogo, limekuwa likisababisha hospitalini hapo kukithiri kwa watoto kujifungua watoto wenzao.



Ofisa Muunguzi kutoka Hospitali ya Wilaya ya Kahama Nyanjura Njuberi, akielezea namna ndoa za utotoni zinavyosababisha kukithiri kwa ongezeko la watoto kujifungua watoto wenzao kwenye hospitali hiyo, kwa vile huzaa katika umri mdogo. **PICHA: MARCO MADUHU**

**WATOTO KUJIFUNGUA**

Mjuberi anatoa takwimu za miaka mitatu mfululizo kuanzia 2017 hadi Machi 2019 zinazoonyesha kuwa watoto 1,171 wameshafika hospitalini hapo kujifungua watoto wenzao.

Anaeleza kuwa kutokana na tatizo la kuozeshwa ndoa za utotoni wengi wao hujifungua kwa upasuaji kutokana na via vyao vya uzazi kutokomaa kikamilifu.

“Mwaka 2017 walijifunga watoto 664, (2018) 416, na (2019) kuanzia januari hadi marchi wameshafika 91, na kufanya jumla yao kufikia 1,171 na hawa ni wale tu ambao wanakuja hospitalini kutokana na kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida. Tunajua kuna wengine wengi ambao hujifungulia majumbani na taarifa zao hazitolewi,”anasema Mjuberi.

“Mtoto mdogo anaposhika ujauzito ni hatari sana kwa afya yake kwani via vya uzazi vinakuwa bado havijakomaa, na wengi wao hujifungua kwa njia ya upasuaji, na kuna wengine wapo kwenye hatari kubwa ya kupoteza maisha kutokana na umwagaji wa damu nyingi,”anaongeza muuguzi huyu.

**USHUHUDA**

Mwanafunzi ambaye jina lake linahifadhiwa mwenye miaka 17 anaye soma kidato cha pili kwa mfumo wa elimu ya watu wazima katika shule binafsi ya Sekondari ya Agape mkoani Shinyanga, anaelezea namna mila na desturi kandamizi zilivyozima ndoto zake.

Alipofaulu kujiunga kidato cha kwanza hakwenda shule bali aliozeshwa ndoa ya utotoni kwa kutolewa mahari ya ng’ombe 19.

Anasema mara baada ya kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2016 akiwa na miaka 14 na kufaulu kuendelea na kidato cha kwanza, baba yake aligoma kumsomesha na kuamua kumtafutia mwanaume wa kumuoza .

Mumewe alitokea mkoani Tabora na hakuwahi kumuona hata siku moja, hadi siku ya harusi yake ndipo akakutanishwa naye akiwa ndani ya shela.

Anaelezea kuwa kutokana na kuwa ni mtoto hakuweza kujitetea wa kike hakuwa na maamuzi ya kupingana na baba yake kutokana na mama yake pia kutokuwa na sauti, hivyo aliridhia tu kuolewa na mwanaume huyo ambaye anamzidi umri sababu ya tamaa ya wazazi wake kutaka mifugo.

“Siku ya harusi nikiwa ndani ya shela naolewa na mwanamume huyo ghafla nikanza kuona watu wanakimbia ovyo, kuja kutaharuki naona polisi wakiwa na Mkurugenzi wa Shirika la Agape, wakitibua ndoa yangu na kunikoa na janga hili la ndoa za utotoni,”anasema muathirika huyo.

“Tangu siku hiyo nilipookolewa kuozeshwa ndoa ya utotoni, baba yangu alinikataa na kunifukuza nyumbani na hataki kuniona hadi leo , ambapo Shirika la Agape mara baada ya mimi kufukuzwa, ndipo wakaamua kunichukua na sasa nasoma kidato cha pili kwenye shule ya sekondari kwa mfumo wa elimu ya watu wazima tofauti na ndoto zangu nilizokuwa nazo,”anaongeza.

John Komba ni Msimamizi wa Mfadhili wa Mradi wa Elimu ya Afya ya Uzazi na Ujinsia kwa Vijana, unaofadhiliwa na Shirika la Sida kutoka Sweden, kupitia Save The Children, mradi ambao utatekelezwa mkoani Shinyanga na mashirika mawili la Kiwohede na Agape, ambao umelenga kutokomeza mimba na ndoa za utotoni.

Anasema mara baada ya kufanyika kwa utafiti mdogo mwaka (2016), waligundua kuwa mkoa wa Shinyanga una tatizo la ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi, hali ambayo imekuwa ikisababisha kuendelea kukithiri kwa wanafunzi kuozeshwa ndoa za utotoni bila ya kujua madharaka yake, ndipo wakaamua kufadhili mashirika hayo ili kutoa elimu hiyo.

“Mradi huu ulioanza mwaka 2017 utasitishwa mwaka huu (2019) na thamani yake ni Sh. milioni 142. Kwa upande wa Shirika la Kiwohede, linautekeleza Kahama Mji, Agape inahamasisha Shinyanga Vijijini ambayo ni maeneo yaliyoathirika sana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni, ili elimu ipate kutolewa na kumkomboa mtoto wa kike kielimu,” anasema Komba.

**CHANGAMOTO**

Ofisa Mradi wa Elimu ya Afya ya Uzazi na Ujinsia kutoka Shirika la Kiwohede wilayani Kahama Amos Juma, anasema katika utekelezaji wa mradi huo wamekuwa wakikumbana na changamoto moja kubwa.

Anaitaja kuwa ni wazazi kuendekeza mila na desturi kandamizi, za kuendelea kuozesha watoto wao ili wapate mifugo.

Anasema licha ya kutoa elimu hiyo ya afya ya uzazi kwa makundi yote ya wazazi pamoja na wanafunzi, bado muitikio wake si mkubwa kwa wazazi kwani kuna baadhi yao ni ving’ang’anzi wa mila hizo.

Lucy Maganga ni Ofisa Mradi wa Elimu ya Afya ya Uzazi na Ujinsia, Shirika la Agape ambapo wanatekeleza mradi huo kata ya Usanda Shinyanga vijijini, anasema mara baada ya kuona mila na desturi ndizo kikwazo cha ndoa za utotoni, waliamua kushirikisha utoaji elimu kwa viongozi wa kimila, dini, vitongoji, kata na madiwani.

Foresta Nkole ni diwani wa Kata ya Usanda Shinyanga vijijini, anakiri alikuwa ni miongoni mwa viongozi ambao walikuwa wakishiri kwenye harusi hizo za ndoa za utotoni, na kubainisha kuwa alikuwa hana elimu ya kutosha juu ya madhara ya ndoa hizo lakini sasa amekuwa mhamasishaji na mpinzani wa mambo hayo..

# KUMEKUCHA NACHINGWEA MNADA WA UFUTA

## ■DC awaonya wakulima, wasigomee bei, tani milioni 1.8 zanunuliwa

Na Sabato Kasika

MSIMU wa ufuta umeanza katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Lindi, huku tani 1,884,000 za zao hilo zikinunuliwa kwenye mnada uliofanyika hivi karibuni katika kijiji cha Mbondo, wilayani Nachingwea.

Kampuni tatu kati ya tisa ambazo ziliomba kununua ufuta katika wilaya za Ruangwa, Nachingwe na Liwale mkoani Lindi kwa njia ya mnada zinatarajiwa kuwa zitanunua jumla ya kilo milioni 1.8.

Katika mnada huo unaosimamiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Runali, bei ya juu ya ufuta ilikuwa Sh. 2,860 huku bei ya chini ikiwa ni Sh. 2,852 kwa kila kilo moja.

Mnada huo ni wa kwanza kufanyika mwaka huu kupitia chama cha Runali, ambacho kinaundwa na vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) kutoka wilaya za Ruangwa, Nachingwe na Liwale.

Wakati mnada huo ukiendelea Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango anatoa neno kwa wakulima ambalo linaweza kuwasaidia kunufai na zao hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango

### USHAURI WA DC

Akizindua mnada huo katika kijiji cha Mbondo, wilayani Nachingwea, Rukia Muwango, anawatahadharisha wakulima wa ufuta kutogomea bei hali, ambayo inaweza kusababisha wakwame hapo baadaye.

Kabla ya kuendelea kuwaonya anawashukuru kwa kukubali kuuza ufuta wao kwa bei hizo, na kisha anawatahadharisha kuhusu madhara ambayo yanaweza kuwapata wanapogomea kuuza mazao yao.

"Mwaka jana kulifanyika mgomo ambao wakulima wengine walifuata mkumbo bila kuamua wenyewe. Matokeo yake yalikuwa kama mtego wa panya wakajikuta wakinasa wenyewe," anasema Muwango.

Anafafanua kwamba madhara ya mgomo huo ni kuathiri vyama vya msingi, vyama vikuu vya ushirika, serikali kuu, halmashauri na baadhi ya wakulima, kwa vile wanakosa wanunuzi wa mazao yao.

"Hivyo kabla ya kushiriki mgomo ni vyema wakulima muanze kufikiria madhara yanayoweza kusababishwa na hatua hiyo ya kugomea bei na kisha mchukue hatua za kuachana nao," anasema.

Anasema serikali mkoani Lindi imekuwa ikitangaza bei elekezi ya ufuta ambayo kimsingi inatakiwa kusimamiwa kwa kuzingatia kwamba inalenga kunufaisha wakulima kulingana na hali halisi ya soko.

Anasema serikali iliamua kuuza ufuta kwa mfumo wa mnada, lakini zikatokea changamoto za baadhi ya wakulima kugomea bei, hali ambayo ameikemea na kutaka isijitokeze katika msimu huu.

"Hatua ya baadhi ya wakulima kugomea bei ilikuwa ni kama mtego wa panya kwani hata wenyewe walijikuta wakikwama, hivyo sitarajii kuona hayo yakijirudia msimu huu," anasema.

### KILIMO CHA UFUTA

Ufuta ni moja ya mazao ya biashara yanayolimwa kwenye mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara an kuwaingizia kipato wakulima wa mikoa hiyo, huku zao kuu likiwa ni korosho.

Hata hivyo, kama ilivyo kwenye korosho, baadhi ya wakulima wamekuwa wakiuza ufuta kwa mitindo wa 'kangoma au chomachoma', ambayo imepigwa marufuku na serikali.

Serikali inapiga marufuku mitindo hiyo, kwasababu inawanyonya wakulima bila wao kujijua na kutajirisha wajanja wachache wanapoenda kujinufaisha kwa jasho la wengine.

Pamoja na juhudi hizo za kuzuia kangoma na chomachoma, bado wapo wakulima wachache ambao hawajaona umuhimu wa kuuza mazao yao kwenye minada huku wakisimamiwa na vyama vya ushirika.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha viongozi wa vyama vya ushirika kuitisha mikutano ya mara kwa mara kwa ajili kuwakumbusha kujiunga na ushirika ili kuepuka kuuza mazao yao kwa bei ya hasara.

### USHAURI WA RUNALI

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Runali, Hassan Mpako, anasema viongozi wa vyama vyote vinavyounda Runali walishapewa maelekezo kwa ajili ya kuwakumbusha wakulima jinsi ya kuuza mazao yao.

"Wanapouza kwenye mnada unaosimamiwa na Runali hawawezi kuibiwa kama ambavyo imekuwa ikitokea kwa baadhi yao, ambao hawazingatii maelekezo ya kutoka kwa viongozi wao," anasema Mpako.

Anasema, katika msafara wa mamba, hata kenge nao hawakosekani, hivyo anaamini kwenye vyama vya ushirika vya msingi, bado kuna wakulima ambao wanakwenda kinyume na utaratibu wa mnada.

Taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa katika mnada uliofanyika kwenye vijiji mbalimbali vya wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, msimu wa mwaka jana, ufuta uliuzwa kati ya Sh. 2,940 hadi Sh. 2,935.

Katika msimu huo kampuni nyingi zilijitokeza na kushinda kununua zao hilo kupitia chama cha Runali huku baadhi zikifanikiwa kushinda tenda hiyo ya ununuzi wa zao la ufuta.

### FAIDA KIAFYA

Wataalam wa afya wanasema kuwa mafuta yana virutubisho muhimu na yamekuwa yakitumika tangu miaka 5,000 iliyopita na kwamba yana maajabu kiafya na pia matumizi ya mafuta hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

Matumizi ya mafuta ya ufuta yamekuwa yakiongezeka kwa kasi na Kwamba umaarufu wake unaongezeka kwa kuwa wengi wanaamini ni dawa kutokana na unafuu utokanao na maradhi mbalimbali, kwamba kuna ukweli uliothibitika kuwa, mafuta ya ufuta yanasaidia matatizo ya ngozi, meno, mifupa pamoja na kuwa na manufaa mengine mengi.

Aidha, wanataja vilivyomo katika mafuta ya ufuta kuwa ni madini ya manganese, shaba, calshamu, chuma, Zinc, thiamine, vitamin B6 , phosphorus, magnesium na protin.



Wakulima wakipembua ufuta.

MAKALA

KATAVI

# Mkoa mpya unaokimbia kwa kasi kufikia maendeleo

**Na Mary Geofrey, Aliyekuwa**

KATAVI

KATAVI ni miongoni mwa mikoa mipya iliyoundwa ndani ya muongo mmoja uliopita. Kipaumbele kwenye maeneo hayo mapya ni kuboresha uchumi na kujiletea maendeleo bila kujali uchanga au upya wa mkoa.

Ukiwa moja ya mikoa iliyo na fursa nyingi za kiuchumi umeendelea kujiimarisha kwenye kilimo, uhifadhi, ufugaji na usafirishaji bandarini, lengo ni kuwekeza na kufikia azma ya maendeleo endelevu.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa Juma Homera, anakutana na wanahabari kutoka vyombo mbalimbali kuzungumzia masuala ya maendeleo kwenye mkoa huo na jinsi ulivyojipanga.

Anausifu mkoa huo kuwa una fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo wanazipigia debe kutekeleza kwa vitendo sera ya kukuza uchumi wa taifa kupitia uwekezaji wa viwanda

Anasema mambo wanayotilia mkazo ni kilimo, ufugaji, utalii na sekta ya bandari ambayo inategemewa kwa kiasi kukibwa kukuza uchumi wa wananchi wa mkoa huo kwa njia ya kusafirisha bidhaa zao kwenda nchi za Zambia na Demokrasia ya Kongo (DRC).



Shehena ya saruji ikipakiwa kwenye bandari ya Kasanga kusafirishwa kwenda nchi za Demokrasia ya Kongo na Zambia hivi karibuni. **PICHA: MARY GEOFREY.**

**SEKTA YA KILIMO**

Homera anasema katika sekta ya kilimo wanazalisha mazao matano ya kimkakati ambayo ni pamba, tumbaku, ufuta, korosho na uvunaji wa asali.

"Tunafanya kilimo kwa zaidi ya asilimia 90 kwa sababu wananchi wamejikita kwenye kulima kibiashara na chakula hasa katika halmashauri ya wilaya ya Mhimbwe ambao wanalima ufuta na mazao mengine bila kuweka mbolea kwa sababu ardhi yake haijachoka," Homera anasema.

Anaeleza zaidi kuwa, wanazalisha mahindi tani 250,000 hadi 400,000 kwa mwaka na mpunga ni zaidi ya tani 350,000 kwa mwaka.

Anaeleza kuwa, katika mwaka 2019/20 wanatarajia kuzalisha ufuta tani 50,000 kwa sababu wana soko la uhakika hivyo wameweka mikakati kwa kila wilaya kuzalisha mazao ya kutosha pamoja na zao la pamba.

Kiongozi huyo wa mkoa anasema pia wana mpango wa kuanza kujikita kwenye korosho na tayari wamepanda zaidi ya hekari 6,000 za mikorosho.

"Kupitia zao hili tunaamini tutafanya biashara katika mkoa wetu baada ya miaka mitatu ambako tutakuwa tumefanikiwa kuvuna," Homera anasema.

Anawataka wawekezaji wa mazao ya chakula na biashara kama ufuta, asali, pamba na nyama kwa sababu bidhaa hizo zinapatika kwa wingi.

Anasema pia kuna fursa za uvuvi katika mkoa huo hivyo wafanyabiashara wanapaswa kuwekeza katika sekta hiyo kwa sababu wanaelekea kwenye lengo kuu la kukuza uchumi.

**SEKTA YA UHIFADHI**

Hifadhi ya Katavi iko juu ya ukanda wenye mafuriko wa Ziwa Tanganyika na ina ukubwa wa takribani kilomita za mraba 4,471 hivyo ni hifadhi ya tatu kwa ukubwa nchini.

Anasema hifadhi hiyo ni maarufu kwa idadi kubwa ya viboko na mamba pamoja na wanyama wengine kama samba na chui.

Anasema wameweka mikakati ya kuendelea kuhifadhi misitu kuhamasisha Watanzania wote wa nje ya mkoa huo kufika katika hifadhi hiyo kwa ajili ya kutembelea.

Homera anawaeleza wadau kuwa, endapo wananchi watajitokeza katika kuona vivutio katika hifadhi hiyo wataongeza mapato ya mkoa huo na kukuza uchumi wa wake.

Asilimia kubwa ya wanaotembelea hifadhi hiyo ni wageni kutoka mataifa mbalimbali , anasema Mkuu wa Mkoa na kwamba pamoja na wanyama hao kuwa kivutio ndani ya hifadhi hiyo, kuna mti ujulikanao 'Mti wa Mzimu wa Katabi.'

Anasema ni mti ambao vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo, vimekuwa vikiutumia kuomba mahitaji mbalimbali kwa mujibu wa imani zao.

Mzimu huo unatajwa kumaliza magonjwa ya mlipuko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo hayo, pia umekuwa ukitumika kuleta mvua kunusuru maisha ya viboko na mamba wanaoishi kwa kutegemea uwepo wa maji katika mto Katuma, anafafanua.

"Katika mti huo wa mkwaju kunakosemekana ndiko mzimu umehifadhiwa, ni mahali makabila mbalimbali ya mkoa huo kama vile Wabende na Wapimbwe, wamekuwa wakifanya matambiko kwa mzimu huo unaoaminika kuishi mahali hapo," anasema.

Kadhalika anasema wana maporomoko ya Sikombe ambayo ni kivutio kikubwa na hifadhi hiyo ina mazingira bora.

Anasema pia wameweka mazingira mazuri ya kuelekea katika hifadhi hiyo kwa kujenga barabara za kisasa ambazo zitawezesha watu kufika hifadhini bila matatizo.

Katika kurahisisha usafiri na watalii kufika katika hifadhi hiyo, anasema wameshakamilisha uwanja wa ndege.

Homera anasema uwanja huo tayari umeshapata kibali cha kurusha ndege hivyo wakati wowote ndege zitaanza kutua kwa ajili ya kufungua milango ya watalii kuingia kwa wingi katika mkoa huo.

Kadhalika anasema tayari wameshanunua gari ya zima moto kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kuwa na uwanja wa ndege wenye vigezo vinavyotakiwa.

UCHUMI WA BANDARI

Mkuu huyo wa mkoa, anasema wana lengo la kuongeza mapato na kujenga bandari ya Karema ambayo itapokea mizigo kutoka Dar es Salaam na Kigoma kwa ajili ya kuivushwa kwenda nchi jirani za Demokrasia ya Kongo (DRC).

Homera anasema bandari hiyo pia itasaidia kupunguza shughuli za malori barabarani ambayo yanaharibu barabara kwa sababu bidhaa nyingi zitakazokwenda Kongo zitapelekwa kwa njia ya maji.

"Kuwapo kwa bandari hii kwa kiasi kikubwa kutasaidia kuokoa fedha ambazo zilikuwa zinatumika kurekebisha barabara zinazoharibiwa na malori," anasema Homera.

MIRADI MINGINE

Anasema pia mradi wa barabara ya kutoka Mpanda Mjini kuenda Kigoma kupitia wilaya ya Tanganyika na ile ya Mpanda kuelekea Tabora ambayo itafungua uchumi wa mkoa huo.

Anasema pia serikali inajenga hospitali katika kila wilaya, vituo vya afya kila kata na zahanati katika vijiji mbalimbali vya mkoa huo kwa lengo la kusogeza huduma za matibabu karibu na wananchi.

Hospitali za wilaya zinajengwa Mlele na Tanganyika na kwamba zitakapokamilika zitasaidia kurahisisha huduma kwa wananchi.

Kuhusu biashara anasema wamewapatia wajasiriamali vitambulisho vya kufanyia biashara na wanaitikia vyema zoezi hilo.

Aneleza kuwa, wamewatumia wafanyakazi wa sekta za umma kufikisha vitambulisho hivyo kwa sababu wananchi walikuwa wakilalamika kukosa huduma hiyo.

"Tumeshawafikia wafanyabiashara wengi na tunaendelea kuwafuatilia, tunaamini kila mmoja akipata kitambulisho ataweza kutambulika na kufanya biashara zake kwa uhuru na nimeshaagiza marufuku kusumbuliwa," anasema Homera.

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi, upinzani waafiki serikali ya mpito

**KHARTOUM,** Sudan

VIONGOZI wa jeshi nchini Sudan, wameafikiana na muungano wa upinzani nchini humo juu ya kuundwa kwa serikali ya mpito ambayo itaandaa njia kwa ajili ya kurejeshwa kwa utawala wa kiraia.

Kwa mujibu wa wasuluhishi, jeshi na upinzani wamekubali kushirikiana katika kuongoza serikali hiyo itakayodumu kwa miaka mitatu na kisha kusimamia uchaguzi huru na wa haki.

Pande hizo mbili zilishindwa kufikia muafaka hapo awali kutokana na mvutano wa kila upande ukitaka uwe na uwakilishi mkubwa zaidi kwenye baraza litakalounda serikali hiyo.

Lakini sasa wameahidi kuunda serikali huru itakayoongozwa kitaalamu pamoja na kuchunguza ghasia za Hivi karibuni zilizosababisha mamia kufariki ni kwa mujibu wa Umoja wa Afrika (AU).

**Pia wamekubaliana kuwa na uchunguzi wa wazi, huru na kina juu ya matukio yote ya ghasia yaliyoikumba nchi hiyo katika wiki za hivi karibuni.**

Taarifa za makubaliano hayo zilipokelewa kwa shangwe mitaani. Sudan imejikuta ikitumbukia katika lindi la ghasia na sitafahamu tangu alipong'olewa madarakani rais Omar al-Bashir kwa mapinduzi ya kijeshi mwezi Aprili mwaka huu.

Mapinduzi hayo yalizaliwa baada ya maandamano makubwa ya raia dhidi ya Bashir, ambaye aliingia madarakani kwa mtutu wa bunduki mwaka 1989.

Siku tatu kabla ya makubaliano hayo ya mpito, makundi makubwa ya waandamanaji wakitaka baraza la kiongozi la kijeshi kuachia ngazi na kupisha utawala wa kiraia.

Watu saba waliuawa na wengine 181 walijeruhiwa katika vurumai hizo, vyombo vya serikali viliripoti.

Mazungumzo ya safari hii yalifanyika jijini Khartoum kupitia usuluhishi uliooongozwa na Waziri Mkuu wa Ethiopia na wanachama wa AU.

"Pande mbili zimekubaliana kuunda baraza huru litakalokuwa na rais wa kupokezana baina ya jeshi na raia kwa kipindi cha miaka mitatu au zaidi," msuluhishi wa AU Mohamed Hassan Lebatt, aliwaambia wanahabari jana Ijumaa asubuhi.

Uchaguzi utafanyika kipindi cha mpito kitakapofikia tamati.

"Pia wamekubaliana kuwa na uchunguzi wa wazi, huru na kina juu ya matukio yote ya ghasia yaliyoikumba nchi hiyo katika wiki za hivi karibuni," aliongeza.

Aidha, walikubaliana kuahirisha kuanzishwa kwa baraza la wawakilishi." Tunaamini kuwa huu ni mwanzo wa zama mpya," alisema Omar al-Degair, kiongozi wa muungano wa wapinzani nchini humo FFC.

Naibu Kiongozi wa Baraza la Mpito la Jeshi TMC, Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, alisema: "Makubaliano haya yatakuwa ni makubwa na hayatamuacha mtu yeyote. Tunaushukuru Umoja wa Afrika na Ethiopia kwa kutuma wasuluhishi na kuwa wavumilivu." **BBC**



Naibu Kiongozi wa Baraza la Mpito la Jeshi TMC, Jenerali Mohamed Dagalo. **PICHA: MTANDAO.**

## AU yakamilisha mkataba biashara huru

**NIAMEY,** Niger

UMOJA wa Afrika wakati wowote kuanzia sasa utazindua awamu ya uendeshaji ya mkataba wa kibiashara barani Afrika uliosubiriwa kwa muda mrefu.

Mataifa 55 ya Umoja huo yatakusanyika kwenye mkutano wa kilele nchini Niger yakijaribu kuondoa ushuru wa biashara miongoni mwa nchi wanachama.

Kundi linalounga mkono mkataba huo huru wa Afrika (AfCFTA), wanaamini kwa kufanya hivyo, biashara baina ya mataifa ya Afrika itaimarika.

Mkuu wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, alisema jana mjini Niamey kuwa hayo ni mafanikio makubwa na yanayoweza kuelezewa kama historia.

Nigeria ilisema itatia saini mkataba huo baada ya kugoma kwa muda mrefu. Mazungumzo kuhusu biashara huru yalianza mwaka 2002 na kungwa mkono na mataifa mengi huku Benin na Eritrea zikiwa za mwisho kutia saini. **DW**



Karanja akiangalia makaburi ya familia yake iliyopotea kwenye ndege ya Boeing Machi mwaka huu. **PICHA: BBC**

# Mfiwa ajali ya ndege akataa fidia ya Boeing

**NAIROBI,** Kenya

MWANAMUME mmoja aliyepoteza familia yake ya watu watano katika ajali ya ndege ya Boeing iliyoanguka nchini Ethiopia mapema mwaka huu amekataa fidia ya shirika la Boeing.

Alisema yeye na familia za waathiriwa wengine wa mkasa huo hawatakubali fidia inayotolewa na kampuni hiyo ya ndege.

Boeing ilisema kuwa itatoa Dola milioni 100 kwa miaka kadhaa kwa serikali za mtaa na mashirika yasio ya kiserikali kuzisaidia familia na jamii zilizoathirika na ajali hiyo ya ndege aina ya 737 MAX nchini Indonesia na Ethiopia.

Malipo hayo yatakayotolewa kwa miaka kadhaa hayatokani na kesi iliyowasilishwa mahakamani baada ya ajali hiyo ambayo ilisababisha vifo vya takriban watu 346.

"Fedha hizo zinalenga kusaidia elimu na maisha ya familia na mipango ya jamii", ilisema Boeing.

Lakini John Quindos Karanja aliyepoteza vizazi vitatu vya familia yake ambayo iliabiri ndege hiyo ya Ethiopia Airlines ikielekea nchini Kenya, alipinga wazo hilo.

Alisema kwamba familia zote zilizopo Kenya na Ethiopia zina kundi moja la WhatsApp ambalo waliliidhinisha siku chache baada ya ajali hiyo.

Karanja alisema kwamba familia hizo hazijapata mawasiliano yoyote rasmi kutoka kwa Boeing na ziligundua habari hizo kutoka kwa vyombo vya habari.

Alieleza kuwa familia zote zilichukua msimamo wa kutoshawishiwa na pendekezo lolote ambalo halijatolewa na mahakama ya haki.

Karanja aliongeza kwamba familia hizo zina habari kwamba kampuni hiyo imekodisha kundi la mawakili ambao wametumwa nchini Kenya na Ethiopia kujaribu kuwasihi kusuluhisha tofauti zilizopo nje ya mahakama.

Alisema hawatakubali hilo na ameongeza kwamba Boeing haina hisia na ni kama inatafuta njia ya mkato kusuluhisha tatizo hilo.

Mkewe Karanja, Ann Wangui Karanja, mwanawe wa kike Carol Karanja na watoto watatu wa Carol Karanja kwa majina Ryan Njoroge, Kellie Pauls na mtoto wa miezi tisa Rubi Pauls walikuwa abiria katika ndege hiyo.

Walikuwa wakisafiri kuelekea Kenya kutoka nchini Canada ambako Carol Karanja na watoto wake walikuwa wakiishi.

Anne Wangui Karanja, alikuwa anarudi nyumbani baada ya kuzuru Canada ambapo alikua amewatembelea wajukuu wake na mwanawe ambaye alikuwa akifanya kazi kama mhasibu katika kampuni moja ya nishati.

Ajali hiyo ya Machi mwaka huu ilikuwa ya pili kuhusisha ndege ya Boeing aina ya 737 Max 8 katika kipindi cha muda wa miezi mitano.

Ndege kama hiyo iliokuwa ikimilikiwa na kampuni ya ndege ya Indonesia carrier Lion Air, ilianguka katika bahari ya Jakarta mnamo mwezi Oktoba 2018.

Wachunguzi wa ajali za ndege wameangazia zaidi mfumo wa kudhibiti ndege hiyo na kampuni ya Boeing imekuwa akishirikiana na wathibiti kuweka mfumo mpya.

Boeing aina ya 737 Max imezuiwa huku kukiwa hakuna tarehe rasmi ya kuruhusiwa kupaa tena. **BBC**

# HADITHI

Kwa sababu kawaida yao huwa hawamfuati msichacha yule wala kumsalimia mpaka yeye aanze kufanya hivyo, hawakufanya chochote bali kumsimama tu na kushangaa. Mwili wa Kadili ndiyo uliokuwa umekufa ganzi zaidi. Kwa akili ya haraka, Meze aliifuata karatasi ile iliyoangushwa kwa bahati mbaya au makusudi kwa mrembo Edina.

# JUMBA JEKUNDU- 8

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

***************************************

Baada ya mazungumzo ya kawaida na mama yake, Kadili alimuomba tena ruhusa mama yake kuwa wikiendi anataka tena kwenda disco.

"Mmh, mwanangu huko disco tutakuwa disco, maana tangu mara ya kwanza nilipokuruhusu kwenda kumekunogea kama vile wanagawa biriani bure, hebu nieleze kuna nini haswa?"

"Mama si tunakwenda tu na Meze kufurahi na kucheza."

"Ndiyo kila wiki, siyo kama zamani mlikuwa mnaweza kwenda kwa mwezi mara moja, au miezi miwili mara tatu, lakini sasa kila wiki vipi?"

Kadili alishtukia sababu ya maswali hayo. Awali alianza kuwa na wasiwasi na mama yake alipomtuhumu kuwa hakuwa kwenye hali yake ya kawaida, lakini sasa anaonekana anauliza sana maswala ya disco kuna nini?

"Inawezekana kuna kitu anakifahamu." Alijiambia.

"Inawezekana mama akawa anafahamu habari za Edina kweli? Nani anamwambia? Na kitu gani anachoambiwa?" Haya ni maswali aliyokuwa akijiuliza.

Kwa mbali alianza kuhisi kuwa kuna mtu anavujisha siri wakati anaongea na Meze. Anachojua yeye ni kwamba hakuna mtu yoyote anayeongea naye zaidi ya rafiki yake kipenzi Meze.

"Ni Meze ndiye anavujisha siri? Hapana". Alijiuliza na kujijibu mwenyewe.

Kwa mbali alianza kuhisi kuwa kuna mtu huwa anasikiliza maongezi yao anapokuwa dukani na rafiki yake. Wakati anawasili nyumbani alikutana na mama mmoja, anaitwa mama Gombea.

Huyu ni mama anayesifika kwa umbea, kutoka maneno huku kupeleka kwingine.

**Ni kama vile alikuwa akizunguka, lakini alijua walipo. Alipofika karibu na Kadili aliinua jicho na kuangalia tena chini. Akatingisha kichwa taratibu kama ishara ya kukataa kitu. Ishara hizi zote zilimchanganya Kadili. Wakati akidhani atafika pale alipo, aligeuka na kurejea alipotoka.**

"Inawekana ni mama Gombea." Alijiambia.

*******************************

Kama kawaida ukumbi wa Blue Star ulijaa watu siku ya wikiendi. Ni mara ya tatu sasa kwa vijana kina Kadili na Meze kufika hapo.

Mara ya kwanza ilikuwa kwa ajili ya kucheza disco. Ya pili ilikuwa ni kumfuata binti mmoja mrembo waliokutana naye mara ya kwanza aitwaye Edina. Hii ni mara ya tatu ilikuwa pia kwa ajili yake.

Kama ilivyo ada, walianza kwa kununua vinywaji na kuanza kunywa taratibu huku walimsubiri mgeni wao kama siku hiyo anaweza kufika. "Tutaonana Mungu akipenda." Kadili aliikumbuka sauti nyororo ya mrembo Edina ilinong'ona kwenye masikio yake.

Hakuna uhakika kama na leo anaweza kufika. Wakati wakinywa na kupiga stori, ghafla aliingia Edina kama kawaida akiwa na wapambe wake.

Alivalia gauni lake zuri la rangi ya bluu, likihanikiza uzuri wake wa asili na rangi yake ya maji ya kunde.

Nywele zake zilikuwa ndefu hadi mgongoni na alizibana vizuri. Kama kawaida yake alionekana ni malkia haswa. Na hata wale waliokuwa wana mazoea ya kufika pale, walikuwa wameshaanza kumtambua msichana huyo.

Hata hivyo kwake haikuwa rahisi kusogelewa na kucheza na mwanaume yoyote zaidi ya yule ambaye amemchagua yeye.

Na siku zote hakuwa mwingine ila ni Kadili. Na hata mabaumsa wake walijua hivyo. Kama kawaida, Kadili hakuwa na ubavu wowote wa kumfuata na kumsalimia, zaidi ya kujiweka vizuri ili aonekane na kufuatwa.

Kwa bahati mbaya siku hiyo hawakuwa sehemu ya kuchezea bali ni ile ya kupata vinywaji, Kadili alikuwa akijiandaa kutaka kutoka pale na kwenda sehemu ya kusakata muziki ambako ndiko mara zote wanakutania.

Wakati anataka kuinua mguu, macho yake yalikutana na ya Edina. Yule msichana mrembo anayemfanya asile, asilale kwa ajili yake, ingawa hajui mwisho wake utakuwa vipi.

Kadili aligundua kuwa kuna kitu ambacho si cha kawaida. Sura ya msichana huyo haikuwa changamfu kama ilivyokuwa mara mbili walizokutana.

Cha ajabu alichogundua ni kama vile msichana huyo hakuonyesha sura ya bashasha kama ilivyokuwa huko nyuma.

Hilo lilimshtua Kadili na alinyong'onyea. Furaha yote ya awali iliisha. Pamoja na kuwa na uhakika kuwa Edina alimuona na macho yakakutana baina yao, lakini aliyaondoa mara moja na hakutaka kuonyesha kuwa amemuoa.

"Kwa nini?" Alijiuliza Kadili huku jasho likimtoka na sura kusawijika. Alipata kusikia kuwa kuna aina ya wanawake ambao hutokea kuwapenda wanaume kwa muda tu, lakini baada ya siku kadhaa anakuwa kama vile hamjui.

"Leo kama vile hayuko vizuri." Sauti ya Meze ilimshtua Kadili aliyekuwa kwenye lindi la mawazo.

Hata rafiki yake naye aligundua hilo.

"Ni kweli Meze, sijui kuna nini?"

"Hebu twende kwenye kwenye ukumbi wa kucheza muziki, anaweza kuja." Meze alimwambia mwenzake.

Waliinuka na kuingia kwenye ukumbi wa muziki, wakaanza kucheza disco. Kadili alicheza lakini mawazo yake hayakuusikiliza kabisa muziki wenyewe.

Alinesa bila mpangilio wowote na kuonekana kama vile mti unaosukumwa na upepo. Hakuna na ukakika kama Edina ataingia kwenye ukumbi wa kucheza muziki kutokana na jinsi alivyo. Alikuwa amenuna.

Ndoto ya Kadili kupendwa na msichana mzuri wa kitajiri ikawa imeyayuka. Kichwani mwake haikuwepo tena. Alichofikiri ni kwamba leo hataki mtu yoyote na pia huenda mpenzi wake yuko nyuma anakuja, hivyo akaona si vema kumfuata kumsalimia.

Kwa mbali alimuona Edina akiingia kwa kunyata na si kwa bashasha kama ambavyo huwa anafanya. Hakuonekana kutaka kucheza.

Aliingia kwenye kundi la watu waliokuwa wanacheza, akinesanesa mithili ya mtu anayecheza, lakini ni kama vile alikuwa anatafuta kitu.

Kama kawaida, mabausa watatu walikaa kando wakimuangalia binti huyo akionekana kujipindapinda kufuatisha mdundo wa muziki.

Ni kama vile alikuwa akizunguka, lakini alijua walipo. Alipofika karibu na Kadili aliinua jicho na kuangalia tena chini. Akatingisha kichwa taratibu kama ishara ya kukataa kitu. Ishara hizi zote zilimchanganya Kadili. Wakati akidhani atafika pale alipo, aligeuka na kurejea alipotoka. Kadili na Meze walishuhudia akiangusha kitu kama karatasi iliyokuwa imekunjwakunjwa kama vile kitu kisicho na thamani, takataka, au karatasi iliyofungiwa kitu cha kula na mlaji akawa amemaliza.

Kwa sababu kawaida yao huwa hawamfuati msichacha yule wala kumsalimia mpaka yeye aanze kufanya hivyo, hawakufanya chochote bali kumsimama tu na kushangaa. Mwili wa Kadili ndiyo uliokuwa umekufa ganzi zaidi. Kwa akili ya haraka, Meze aliifuata karatasi ile iliyoangushwa kwa bahati mbaya au makusudi kwa mrembo Edina.

Kadili yeye macho yake yalikuwa yakimsindikiza mrembo Edina ambaye alionekana hakuwa kwenye hali ya kawaida, akitoka moja kwa moja kwenye ukumbi huo huku mabausa wakimfauta kwa nyuma.

**Itaendelelea Jumamosi**

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO


**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz ,au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Faustine Titus Dumla** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0895-0039** kilichotlewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Mwaya. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **KLR/RB/3254/2018**

115310301

## KUPOTEA KWA CHETI



**JUSTERRAHEL ONESMO MACHA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari MARINGENI chenye **Index No S-2028-0019** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2016
Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa polisi: **MOS/RB/4217/19**

115311102

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA SIMANJIRO.**
**WILAYA YA SIMANJIRO**

**MAOMBI NA. 89/1219**

**EVELYIN GILEAD SHANGALI**
**(Suing as an estate administrati)........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**EXCELLENTCOM TANZANIA LIMITED......MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: EXCELLENTCOM TANZANIA LIMITED**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Simanjiro.Shauri limepangwa kutajwa tarehe 16/07/2019 saa mbili na nusu(2:30)asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.Silas, hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako.
**ANGALIA:** Kama hutohudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo 01 mwezi Julai, 2019.

115311202

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: MAGOMENI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 252/2019**

**Ombi la ABDULKADIR RWEYEMAMU MBEO kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MARIAM ABDULKADIR KOKWIJUKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 26/07/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 3/07/2019

115310802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOHN FELIX MAPANDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T. 199 DCV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/108255/2019.**

115311702

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki iliyokuwa na namba ya usajili **T 129 CHB** na chasis namba **MD2A21BZ0CWJ39380.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IR/TR/RB/2053/2019**

115311302

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**HAMADI JOSHUA SHOMARI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T225 DKX. REG NO. 7522044.** CHASSIS NO. **ZRT 26030117893.** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **AR/RB/6311/2019.**

115310402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ISSAH JUMA RASHID** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya FECON yenye namba za usajili **MC 835 BEZ.** Chassis namba **LDAPAJOB4GGB01845**. Engine namba. **155FM1216F01845** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB3518/2017**

115310702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA DODOMA**

**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI Na 179 YA2019 BAINA YA**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC ..............MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **GODFRRID MICHAEL MUSHI**
2. **ALFRED ANSELIM KINABO**

**KWA : GODFRRID MICHAEL MUSHI**
**ALFRED ANSELIM KINABO**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 1/08/2019

**Angalizo:** kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri wa Baraza hili leo mwezi wa juli 2019

115310502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**OSCAR GODFREY MTENDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISH yenye namba za usajili **T 195 BDX** rangi ya white/green. Chassis namba **FE637EV501272.** Engine namba. **4D33D82825.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/23880/2016**

115310601

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;139/2019**

**Ombi la BERNARD BEREGE CHENEMIAGE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FRANCIS JUMA BEREGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/07/2019.

115310902


*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*
*Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*
*0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# LEICESTER CITY YAFANIKIWA KUMSAJILI PEREZ

**LEICESTER,** England

KLABU ya Leicester imetangaza kumsajili, Ayoze Perez kwa pauni milioni 30 kutoka Newcastle.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekubali kusaini mkataba wa miaka minne na miamba hao wa uwanja wa King Power.

Perez amekuwa mchezaji wa pili kusajiliwa katika kipindi cha majira ya joto baada ya kumchukua,James Justin kutoka Luton.

Nyota huyo wa Hispania alitumia misimu mitano pale kwenye dimba la St James' Park na msimu uliopita ulikuwa mzuri zaidi kwake baada ya kufunga mabao 12.

Akizungumza na televisheni ya LCFC TV, alisema: "Nina furaha kubwa na nimeridhishwa mno. Najisikia fahari kuwa sehemu ya kikosi cha Leicester na sitasubiri kuanza kucheza.

"Klabu inataka kukua kadiri inavyowezekana na hicho ndio kitu ninachokipenda. Nilizungumza na kocha na hilo ndilo alilolisema kuwa jambo muhimu zaidi.

"Na hali hii inanipa hamasa kubwa zaidi ya kufanya maamuzi ya kuendelea kucheza hapa."

Naye kocha wa Leicester, Brendan Rodgers alisema: "Nafikiri Ayoze atakuwa mchezji muhimu zaidi kwa kikosi chetu. Kwa sababu ni mwepesi na mwenye kasi kubwa dimbani, ana uzoefu wa kutosha kwenye Ligi Kuu England."

# Mke ampeleka Icardi Juve

**TURIN,** Italia

MKE wa mshambuliaji wa Inter Milan, Mauro Icardi ambaye pia ni wakala wake, Wanda Nara yupo kwenye mazungumzo na Juventus ili kukamilisha usajili wa nyota huyo.

Wanda ameripotiwa kwenda Ibiza Jumanne iliyopita kukutaka na bosi wa Juventus, Fabio Paratici kuhusu dili la mshambuliaji huyo kabla hajarudi zake Milan kumalizana na Inter Milan.

Kocha mpya wa Inter Milan, Antonio Conte, anataka kumpiga bei Icardi ili kupata fedha za kumnasa mshambuliaji wa Manchester United, Romelu Lukaku.

Kocha huyo ameshamwambia Icardi kwamba hatakuwa kwenye mipango yake ya msimu ujao licha ya kwamba amefunga mabao 40 kwenye ligi kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita.

Inter wanahitaji pauni milioni 54 kwenye mauzo ya mchezaji huyo, ambaye alivuliwa unahodha na kuwekwa nje ya kikosi sehemu kubwa ya msimu uliopita kutokana na utovu wa nidhamu.

Kocha mpya wa Juventus, Maurizio Sarri ni shabiki mkubwa wa Icardi na alijaribu kutaka kumsajili wakati alipokuwa akiinoa Napoli.

Conte anataka kutumia fedha za kumuuza mshambuliaji huyo ili kumsajili Lukaku na mabosi wa timu hiyo wameshapanga vikao na mawakala wa mchezaji huyo.

United walikataa ofa ya pauni milioni 62, ofa ya mkopo wa miaka miwili iliyoletwa mezani kwao na Inter kwa ajili ya huduma ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer hana pingamizi la kumuuza Lukaku, lakini anataka fedha za kutosha ili na yeye aweze kufanya usajili wa wachezaji wapya.




# Paulo Dybala atumiwa kumhamisha Pogba




**TURIN,** Italia

KATIKA harakati zake za kutaka kumnasa Paul Pogba klabu ya Juventus sasa inataka kumtumia Paulo Dybala kama chambo ya kumnasa nyota huyo.

Pogba ambaye anakipiga pale klabu ya Manchester United anataka kuondoka hapo kwenye dimba la Old Trafford, huku mashetani wekundu hao wakihaha kutaka kumbakisha.

Juvetus wanataka kumtumia Dybala baada ya wapinzani wao katika mbio za kumsajili Pogba, Real Madrid kuwa tayari kuwapa United mshambuliaji wake, Gareth Bale. Dybala anaweza kupisha njia kwa sababu kocha mpya wa Juventus, Maurizio Sarri ameamua kumrudisha mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Gonzalo Higuain ambaye alitolewa kwa mkopo kwenda Chelsea dirisha la Januari.

Beki Sandro na kiungo Blaise Matuidi nao wanaweza pia kutumika katika dili la kumrudisha Pogba ambaye aliuzwa klabuni hapo kwenda Old Trafford katika dirisha la uhamisho la mwaka 2016 kwa dau la rekodi ya dunia pauni milioni 89.

Mabosi wa United hawataki kuachana na Pogba kwa sababu za kibiashara lakini kocha wa timu hiyo, Ole Gunnar Solskjær yuko radhi kuachana na kiungo huyo.

HABARI MICHEZO

# De Jong: Furaha yangu ni kucheza na Messi




**BARCELONA,** Hispania

FRENKIE de Jong amefanya mahojiano yake kwa mara ya kwanza tangu awasili Barcelona, ambako alikwenda kukamilisha vipimo vya afya kabla ya kukamilisha uhamisho wa euro milioni 86 ambao ulikubaliwa tangu Januari mwaka huu.

'Dogo' huyo wa Uholanzi alitarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano kuwachezea La Blaugrana hao baada ya kuwa na misimu mitatu mizuri na Ajax, ambako ameichezea mechi 89 katika mashindano yote na kufunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho 13.

Akiwa amenukuliwa na tovuti ya Klabu ya Barcelona, De Jong alibainisha: "Nina furaha kubwa kuwa hapa hatimaye. Tangu nikiwa mdogo nilikuwa na ndoto ya kuichezea Barça, na sasa nipo hapa ni jambo nzuri.

"Nina furaha kubwa zaidi kuwa hapa kucheza na Lionel Messi, kwani nimekuwa nikimfuatilia mara zote. Sasa ni wakati mzuri zaidi kucheza nae pamoja kwenye timu moja."

"Natarajia kuwa na wakati mzuri zaidi kwenye maisha yangu ya soka hapa katika Uwanja wa Camp Nou ambako nitakuwa nacheza kwa mara ya kwanza.

"Nina uhakika kwamba nitakuwa na kipindi kizuri zaidi kwa muda wote nitakaocheza hapa na nina matumaini makubwa ya kuisadia klabu yangu," alisema.

Jana Ijumaa De Jong alifanyiwa vipimo vya afya yake kabla ya kusaini mkataba wa kuitumikia klabu hiyo.

# MARCELO AGONGANISHA VIGOGO ULAYA




**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kwamba imetoa ofa kwa beki wa kushoto wa Brazil, baada ya nyota huyo kuomba kuondoka pale Real Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa pale kwenye dimba la Bernabeu kwa misimu 13, akishinda mataji manne ya Ligi Kuu Hispania, La Liga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini kutokana na kwa sasa kutokuwa na uhakika wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza, huku akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara, Marcelo ameomba kuondoka.

Kocha, Zinedine Zidane ameshabainisha wazi kwamba beki huyo hayupo kwenye mipango yake na hasa baada ya mwezi uliopita kumnunua Ferland Mendy kutoka Lyon kwa pauni milioni 47.

Marcelo baada ya kuomba kuondoka klabuni hapa, amekuwa akipata ofa kadhaa kutoka Klabu mbalimbali Ulaya, kwa mujibu wa gazeti la Hispania la Marca. Kwa sasa Arsenal ndio inayotajwa kuwa kwenye mbio za kutaka kumsajili mchezaji huyo huku wakishindana na Paris Saint-Germain, Juventus na AC Milan.

Aidha taarifa zaidi zinasema kwamba, Marcelo alikuwa na mpango wa kufanya mazungumzo na rais wa Real Madrid, Florentino Perez.

Marcelo kwa sasa yupo likizo baada ya kuachwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Brazil ambacho kimetinga fainali ya michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, na kitacheza na Peru kesho Jumapili.



# Ander Herrera rasmi PSG

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya PSG imethibitisha kwamba, imekamilisha usajili wa kiungo wa Manchester United, Ander Herrera.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alitaka kumbakisha kiungo huyo raia wa Hispania wakati huu akiwa anaijenga timu yake, lakini alishindwa kumshawishi kusaini mkataba mpya hapo Old Trafford.

Klabu hiyo ya Ufaransa ilitangaza kumsajili mchezaji huyo kwa uhamisho huru na ametajwa kwamba atakuwa akilipwa kiasi cha pauni 300,000 kwa wiki.

Herrera alikuwa na namba ya kudumu katika kikosi cha United msimu uliopita na ametua PSG kwa ajili ya kwenda kuziba pengo la Adrien Rabiot aliyetimkia Juventus.

Ameiambia tovuti ya klabu hiyo kuwa: "Paris Saint-Germain ni Klabu kubwa nchini Ufaransa.

"Inakufanya uzidi kuimarika kama mchezaji na kwa uhakika ni wakati mzuri kwangu kuvaa jezi ya PSG na naamini nitakuwa na wakati mzuri kwenye Klabu hii."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BUFFON RASMI AREJEA JUVENTUS

●●● Ajiandaa kwenda kuvunja rekodi ya mkongwe Maldini katika ligi hiyo ya Serie A...

**TURIN,** Italia

GOLIKIPA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Buffon, amekamilisha mchakato wa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Juventus.

**Buffon, ambaye ana umri wa miaka 41, aliwatumikia vigogo hao wa Turin kwa muda wa miaka 17 kabla ya kujiunga na Paris St-Germain ya Ufaransa msimu uliomalizika.**

Mlinda mlango huyo ambaye Juni 5 mwaka huu, alitangaza kuondoka PSG baada ya kuichezea kwa msimu mmoja, juzi asubuhi alikuwa Juventus kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Mkongwe huyo amesaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuichezea klabu hiyo maarufu Bianconeri, ambayo sasa iko chini ya kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri.

Golikipa huyo wa zamani wa Italia, ambaye ameshinda mechi 176 akiwa na taifa hilo, ni mmoja wa wachezaji ambao wanatajwa kuwa na uwezo wa kubadilisha mchezo.

Mshindi huyo wa taji la Kombe la Dunia za mwaka 2006, Buffon ameshinda mataji tisa ya Ligi ya Serie A pamoja na manne ya Kombe la Italia, pia ameshinda taji la Ligi Kuu Ufaransa msimu uliomalizika.

Buffon anahitaji mechi nane tu za Serie A ili kuvunja rekodi ya kucheza mechi 647 ambazo zinashikiliwa na mkongwe wa AC Milan, Paolo Maldini.

Buffon ni mchezaji wa tatu wa Juventus ambaye yuko huru katika kipindi cha majira ya joto akifuatiwa na Aaron Ramsey ambaye ameondoka Arsenal na Adrien Rabiot aliyepewa baraka za kuondoka Paris St-Germain.

Kwa mara ya kwanza Buffon alijiunga na Juventus akitokea Parma mwaka 2001 na kudumu klabuni hapo hadi mwaka 2018, akishinda mataji 12 mfululizo ya Serie A.

Hata hivyo, mkongwe huyo ameshindwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na vigogo hao, akipoteza mechi tatu za fainali.

Msimu uliopita, Buffon sambamba na Claudio Marchisio, ambaye alikuwa klabuni hapo tangu mwaka 2005, waliondoka Juve, wakati Andrea Barzagli yeye alitangaza kustaafu, na kuifanya idadi ya wachezaji wanaoifahamu vema klabu hiyo kupungua.

## ZISIKUPITE

### CITY YAACHANA NA MAGUIRE

MANCHESTER City haiko tayari kukutana na Leicester kwa ajili ya kufanya mazungumzo kuhusu beki, Harry Maguire wakati mahasimu wao Manchester United wao wameonyesha wameweka nguvu kuhakikisha wanashinda mchakato wa kupata saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(90Min)***

### FERNANDES KIMEELEWEKA

NYOTA anayewindwa na Manchester United, Bruno Fernandes tayari ameshakaribia kukamilisha mchakato wa kutua Old Trafford. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 kutoka Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya UIreno tayari ameshatua Manchester kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya. ***(Sport Witness)***

### NIGUEZ KUMRITHI POGBA

MANCHESTER United maarufu The Red Devils imemtaja beki wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Saul Niguez (24), ndiye mrithi wa Kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba (26), ambaye anatarajia kuondoka klabuni hapo. ***(Express)***

### SCHUBERT AIKATAA ARSENAL

KLABU ya Arsenal itamkosa golikipa Mjerumani Markus Schubert, ambaye ana umri wa miaka 21 kwa sababu ameamua kujiunga na klabu ya Schalke akitokea Dynamo Dresden. ***(Sport1)***

### ARSENAL YAMWANIA MARCELO

ARSENAL iko katika vita ya kuwania saini ya beki wa kushoto Mbrazil Marcelo (31), ambaye ameambiwa na Real Madrid ajipange kuondoka. ***(Sport - via Metro)***

### LUKAKU ANUKIA MILAN

INTER Milan inaendelea na mchakato wa kuwasilisha rasmi ofa ya kutaka kumsajili straika wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Sun)***

### RONDON AWINDWA

WETS Ham imejiimarisha ili kuongeza nguvu za kumwania straika wa Newcastle na Timu ya Taifa ya Venezuela, Salomon Rondon (29) kwa kuongeza dau. ***(Star)***

### LOVREN KUONDOKA LIVERPOOL

NYOTA Dejan Lovren anajiandaa kuondoka Liverpool baada ya AC Milan inayoshiriki Ligi ya Serie A kuanza mchakato wa kumwania beki huyo wa Timu ya Taifa ya Croatia ambaye ana umri wa miaka 30 ili atue San Siro. ***(Mirror)***

### CITY, JUVENTUS VITANI

MANCHESTER City inatarajia kukutana na ushindani kutoka kwa Juventus kwa ajili ya kuwania saini ya beki wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sport English - via Mirror)***

### SILVA KUMTOA NEVES

INTER Milan inataka kumtumia straika wa Ureno, Andre Silva (23), kuwa sehemu ya usajili wa kiungo wa Wolves Mreno Ruben Neves (22), ambaye dau lake limetajwa kuwa ni pauni milioni 40.3. ***(Sport Mediaset - in Italian)***

HABARI MICHEZO

# Zimamoto yaota ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Zimamoto umesema kuwa utakiandaa vema kikosi chao kwa sababu wamedhamiria kufanya vema katika msimu ujao wa Ligi Kuu Zanzibar, tofauti na ilivyokuwa katika msimu uliomalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Zimamoto, Ali Jongo, alisema kuwa wameandaa programu nzuri ambazo zitawafanya wachezaji wao wame imara na tayari kukabiliana na ushindani.

Jongo alisema kuwa licha ya kuchelewa kuanza mazoezi, Zimamoto imejipanga kufanya vizuri na lengo lao kuu likiwa ni kuutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambao msimu uliopita "hesabu" zao zilipotea kidogo.

Kiongozi huyo alisema kuwa tayari wachezaji wao wameshaanza mazoezi, ambapo kwa siku wanafanya mara moja, lakini wakitarajia kuongeza "dozi" hiyo itakapofika mwishoni mwa Julai.

"Kwa sasa timu inafanya mazoezi mara moja kwenye Uwanja wa Ngome Fuoni, na mazoezi yanaendelea vizuri hadi sasa hakuna mchezaji aliyeumia mazoezini na inabidi kutupata matumaini sisi viongozi wa timu kuwa timu yetu msimu huu itanyakuwa ubingwa au kumaliza nafasi ya pili," alisema Jongo.

Aliongeza kuwa katika kuimarisha kikosi hicho, pia wanatarajia kusajili wachezaji wapya wanne na wataangalia zaidi nyota waliong'ara kutoka kwenye timu za Ligi Daraja la Kwanza ngazi ya Kanda na Daraja la Kati maarufu Central.

"Nafasi ambazo tutaziimarisha ni katika idara ya ushambuliaji, hapa tutasajili wawili na walinzi pia watakuwa wawili, muda ukifika, tutaweka wazi kila kitu kuhusu wachezaji hao," Jongo alisema.

Zimamoto ilijiondoa katika mbio za ubingwa wa ligi hiyo msimu uliomalizika baada ya kupoteza michezo miwili ya mwisho na kwa matokeo hayo, ilimaliza msimu ikiwa katika nafasi ya tatu nyuma ya KMKM na JKU.

# TFF YAZIKUMBUSHA KLABU, NYOTA BARA KUJITAMBUA

**Na Shufaa Lyimo**

ILI kujiepusha na adhabu, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) limevitaka vilabu vyote nchini kuwa makini katika kufanya usajili wa wachezaji wao kwa lengo la kuepusha matatizo yanayojitokeza wakati dirisha la usajili huo litakapofungwa, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema kuwa shirikisho hilo litasikitika kukuta kuna klabu imefanya usajili bila ya kukamilisha taratibu za mchakato huo ambao ndio hutoa taswira ya timu husika.

Ndimbo alisema kuwa TFF imetoa muda mrefu kama ambavyo nchi nyingine hufanya, kwa lengo la kutaka kila klabu ikamilishe mchakato huo kwa kuzingatia kanuni na taratibu.

"Tunasisitiza klabu zote zifuate taratibu za usajili, kwa sababu dirisha la usajili litakapofungwa, kusiwe na mapungufu ya baadhi ya usajili wa wachezaji kutokamilika, kila klabu iweke viambatanisho vyote muhimu, vinavyotakiwa kutokana na aina ya usajili wa mchezaji husika," alisema Ndimbo.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa, hali hiyo itasaidia kurahisisha mchakato huo, na kila mchezaji kupata timu ya kuitumikia na si kuona baadhi wanakosa klabu kwa makosa yanayojirudia kila msimu.

"Huu ni wakati wa klabu kuhakikisha mchezaji wanayemsajili, anakuwa na mkataba halali, ambao umetimia na umeridhiwa na pande zote mbili,"alisema Ndimbo.

Wakati huo huo, Ndimbo, aliwataka wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania ( Taifa Stars) ambao wamerejea nchini jana kutoka Misri kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika( Afcon) wasikatishwe tamaa na matokeo waliyopata na badala yake waelekeze akili zao kwenye mashindano yajayo.

"Vijana wetu wa Taifa Stars wamejitahidi kwa sababu ni miaka mingi tulikuwa hatujashiriki Afcon,naomba Watanzania wasiwalaumu wachezaji bali wamuachie hiyo kazi mwalimu ambaye ndio alikuwa na timu ,"alisema Ndimbo.

Taifa Stars ambayo inanolewa na Mnigeria Emmanuel Amunike sasa hivi itaanza kujiandaa mechi za kuwania tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambapo itaanza kwa kuwakaribisha Sudan ifikapo Julai 26 mwaka huu.



Nahodha wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta (kulia), akiweka sahihi kwenye mkono wa mchezaji wa karate wa Kituo cha Michezo cha Petrosport kilichoko Cairo, Misri. Stars ilikuwa inafanya mazoezi kwenye Uwanja wa Kituo hicho ambao unamilikiwa na klabu ya Petrojet, inayoshiriki Ligi Kuu Misri. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Seseme, Shomary wasajiliwa Kagera*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inakuwa imara na kurejea kwenye ushindani, uongozi wa Ligi Kuu Tanzania Bara umetangaza kuwasajili wachezaji watatu wapya kwa ajili ya msimu ujao, imeelezwa.

Nyota ambao wametangazwa kutua Kagera Sugar jana kuwa ni pamoja na Abdallah Seseme kutoka Mwadui FC ya mkoani Shinyanga, Ally Shomary wa Mtibwa Sugar na Zawadi Mauya ambaye alikuwa akiitumikia Lipuli FC ya Iringa.

Meneja wa Kagera Sugar, Mohammed Hussein, aliliambia gazeti hili kwamba wamejipanga "kukisuka" kikosi chao kwa sababu hawataki kuona wanaendelea kuwa kwenye wasiwasi wa kushuka daraja kama ilivyotokea kwa misimu mitatu iliyopita.

Hussein alisema kuwa licha ya kusajili wachezaji wa ndani tu, wanaamini Kagera Sugar itaendelea kutoa ushindani kwa klabu kongwe, lakini ikidhamiria kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tumeshaanza kukisuka upya kikosi chetu, tunatarajia ushindani utaongezeka tena katika msimu unaokuja kama ambavyo inaonekana, kila timu inajiimarisha kwa sababu haitaki kuwa kibonde, tunasajili kulingana na mahitaji yetu na si kuangalia wengine wanafanya nini, tunaamini wachezaji hawa tunaowasajili, watasaidia kutimiza malengo yetu," alisema kiongozi huyo.

Aliwataja wachezaji wengine ambao waliwasajili tayari kuwa ni Evarist Mujwahuki kutoka Mbao FC ya jijini Mwanza, Erick Kyaruzi na Frank Ikobeki, wote kutoka Mbeya City.

Msimu uliomalizika, Kagera Sugar inayofundishwa na Mecky Maxime, ilinusurika kushuka daraja baada ya kuwafunga Pamba FC ya Mwanza mabao 2-1 katika mchezo wa marudiano wa Play Off kufuatia sare ya bila kufungana katika mchezo wa kwanza.

# Michezo

Jumamosi Julai 6, 2019

Nipashe




Buffon rasmi arejea Juventus

UKURASA 30

# Mkwabi afunguka sintofahamu Simba

## ●●● Ashangazwa kuhusika kuhujumu klabu hiyo pamoja na mgawanyiko uliopo...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wingu na hofu limeendelea kutanda ndani ya Simba kufuatia sintofahamu iliyopo kati ya viongozi na mwekezaji wa klabu hiyo, mfanyabiashara maarufu nchini, Mohammed Dewji "MO", kiongozi mkuu wa mabingwa wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Swedi Mkwabi, ameibuka na kusema naye anashangazwa na hali hiyo iliyopo.

**Hofu ya "ndoa" kati ya MO na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kutaka kuvunjika ilianza kuzungumzwa zaidi ya miezi miwili na taarifa za ndani zinaeleza kuwa hali hiyo imekuja kutokana na kuwapo kwa tofauti kati ya viongozi na mwekezaji huyo wa klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.**

Hali ilizidi kuwa mbaya baada ya MO kuanza kuandika mfululizo wa ujumbe mbalimbali zenye "mafumbo" katika kurasa zake za kijamii na kuzidisha mijadala miongozi mwa wanachama, mashabiki wa Simba na wadau mbalimbali wa soka hapa nchini.

"Kwenye uongozi, na kwenye maisha, huwa nakaribisha kukosolewa. Lakini siwezi na sikubali kufanya kazi na mtu anayejuhumu malengo, mipango na maslahi mapana ya taasisi, mtu anayetoboa mtumbwi tunaosafiri nao," MO aliandika ujumbe huo katika ukurasa wake huku akiweka picha inayomwonyesha Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kushoto) na kulia ni Mwenyekiti wa Simba, Swedi Mkwabi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwabi, alisema kuwa hata yeye binafsi haelewi sintofahamu hiyo iliyopo ndani ya klabu yao ambayo kwa sasa iko kwenye mchakato muhimu wa kukamilisha usajili kwa lengo la kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao.

Mkwabi alisema kuwa kama kiongozi mkuu, hafurahishwi na hali hiyo kwa sababu haileti "afya" ya maendeleo ya klabu yao na mpira wa miguu hapa nchini.

Hata hivyo, Mkwabi alisema kwamba anasikitishwa zaidi kuona yeye akihusishwa katika sintofahamu hiyo, bila ya kufahamu sababu za msingi.

"Hata sielewi, hata mimi ninashaa, ninatajwa kuhusika kushirikiana na ( majina tunayahifadhi) ili kuzuia mambo yao," alisema kwa kifupi kiongozi huyo ambaye aliingia madarakani katika uchaguzi wa klabu hiyo uliofanyika Novemba mwaka jana chini ya katiba mpya ambayo imempa nguvu mwekezaji asilimia 49 na asilimia 51 zimebakiwa kwa wanachama.

Taarifa za ndani za klabu hiyo zinasema kuwa moja ya sababu ambazo zimepelekea pande hizo mbili kutofautiana, ni kutofanya uamuzi wa pamoja wa mambo mbalimbali yanayoihusu timu yao, ikiwamo suala la usajili wa wachezaji wapya na wale wa zamani, wanaopewa mkataba mipya.

Imeelezwa kuwa, mchakato wa usajili unaendelea klabuni hapo, umesaidia kuwatuliza wanachama ambao wanaamini ujio wa mwekezaji huyo, ulichangia kwa kiasi kikubwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika.



Mchezaji wa Bournemouth, Simon Francis (katikati) akiwa katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu England, huku akifuatiliwa na wasimamizi wa klabu hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Gadiel azidi kuivuruga Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

IKIWA leo ndio siku ya mwisho ambayo beki, Gadiel Michael, amewapa viongozi wa Yanga kukamilisha mahitaji yake anayoyataka, uongozi wa klabu hiyo umemtaka mchezaji huyo achague timu anayoitaka kuitumikia katika msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Dismas Ten, alisema bado wanaendelea kuzungumza na Gadiel ili aweze kusaini mkataba mpya, lakini ameweka wazi kwamba beki huyo yupo kuchagua klabu anayotaka kuitumikia.

"Gadiel yupo huru, kwa sababu mkataba wake umeisha tangu mwezi uliopita, sisi kama Yanga tulimpa nafasi ya kuchagua timu anayoitaka, kwa hiyo ni ngumu kuzungumzia suala lake kwa sasa,"alisema Dismas.

Kiongozi huyo aliwataka mashabiki wa Yanga kutokuwa na wasiwasi kwa sababu klabu yao imeshasajili wachezaji wazuri ambao wataongeza ushindani ndani ya klabu hiyo katika msimu ujao.

Alisema kuwa kikosi chao kinatarajia kuanza mazoezi kesho baada ya wachezaji wao waliokuwa likizo na wale wapya kutarajia kuripoti jijini.

"Leo (jana) tunatarajia kuanza kupokea wachezaji wetu ambao wanatoka mikoani na wale wa kimataifa kwa ajili ya kujiandaa kuanza rasmi mazoezi Jumapili, ila tunatarajia kutangaza programu zetu zitakavyokuwa kuanzia Jumatatu baada ya taratibu kukamilika," aliongeza kiongozi huyo.

Hata hivyo, taarifa za ndani zilizopatikana jijini zinaeleza kwamba beki huyo wa zamani wa Azam FC, tayari ameshasaini mkataba wa kuitumikia Simba na kinachosubiriwa ni muda rasmi wa kutangazwa.

"Muda tu ndio utaongea, kiukweli tayari Gadiel alishasaini Simba, ila huu utaratibu wao mwaka huu, umejua kuwaweka wanachama roho juu," alisema mmoja wa viongozi wa juu wa Yanga.

Alisema nyota huyo amekuwa akiwazungumzia viongozi wake kama ambavyo aliyekuwa mshambuliaji wao, Ibrahim Ajibu, alivyokuwa anafanya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002